SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI

**MHESHIMIWA**
***Dkt.* Khalid Salum MOHAMED**
**(MBM)**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026-2027

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2026**

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI**
**Dkt. Khalid Salum MOHAMED (MBM).**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI – ZANZIBAR**

**KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2026**

**VIONGOZI WA WAKUU WA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**



**Mhe. Dkt. Khalid Salum MOHAMED (MBM)**
**Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi**
**Zanzibar**



**Mhe. Badria Atai Masoud**
**Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi**
**Zanzibar**

## YALIYOMO

**YALIYOMO**............................................................................ii

**ORODHA YA VIAMBATANISHO**......................................................v

**A.UTANGULIZI** ........................................................................1

**B.MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA.** .....................................3

**C.VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2025/2026.**..........................................................................................4

**D.UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026**................................................................5

D.1. Mapato yaliyokusanywa na Wizara kwa Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026..................................................5

D.2. Fedha zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ................................................................6

D.3. Utekelezaji wa Malengo ya Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ..................................7

**PP0101- PROGRAMU YA USAFIRISHAJI.**........................................7

SP010101 - Programu Ndogo: Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji. ..................................................7

**PP0105 - PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO.** .........................21

SP010501 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo...........................................................................21

**PP0104 - UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI** ..........................................24

SP010401- Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ...............................................................25

SP010402 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango,Sera na Tafiti za Wizara ...............................................................26

SP010403 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ........................................................ 29

**E.UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULA 2025 HADI MACHI, 2026 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2026/2027. ...................... 30**

E.1. SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR .................................... 30

E.2. SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR .................................................. 36

E.3. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR ...................... 39

E.4. MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR .......................................................................... 45

E.5. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR ............ 49

E.6. BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO .................................................. 54

E.7. BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI............................... 57

**F.MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO ............................ 60**

**G.MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA UJENZI NA UCHUKUZI. ........................................................ 60**

**H.MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027. ............................................................................ 61**

H.1. Vipaombele Vikuu vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ............................................................ 61

H.2. Programu za Wizara na Malengo ya kila Progamu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. ......................................... 63

**P01- PROGRAMU YA UJENZI NA MIUNDOMBINU YA BARABARA ............................................................................ 64**

S0104 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Barabara ........................................................................ 64

S0105 – Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo....68

**P02 - PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA UCHUKUZI. ....70**

S0201 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombini ya Uchukuzi (Anga na Baharini )....70

S0202 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama .... 71

**P03 - PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA ....73**

S0301 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ....74

S0302 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ....75

S0303 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ....76

**I.HITIMISHO ....77**

**J.MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027....80**

## ORODHA YA VIAMBATANISHO


**KIAMBATANISHO NAMBARI 01:** Ufafanuzi wa Mapato yaliyokusanywa kwa Mwaka wa Fedha 22025/2026....................82

**KIAMBATANISHO NAMBARI 2A:** Fedha za Matumizi ya Kawaida Maendeleo Kwa Programu Kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ..............................83

**KIAMBATANISHO NAMBARI 2B:** Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026..........................................84

**KIAMBATANISHO NAMBARI 3A.** Orodha ya Barabara zilizokamilika kwa Kiwango cha Lami/Zege kwa kila Mradi kwa Kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026....................85

**KIAMBATANISHO NAMBARI 3B.** Orodha ya Barabara zilizokamilika kwa Kiwango cha Lami/Zege kwa Kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026 kwa kila Mkoa ............................88

**KIAMBATANISHO NAMBARI. 4A** Utekelezaji wa Kazi za Uandaaji wa Nyaraka za Ujenzi, Miezi Tisa Mwaka 2025/2026.....................90

**KIAMBATANISHO NAMBARI 4B:** Utekelezaji wa Kazi za Usimamizi za Ujenzi, Miezi Tisa Mwaka 2025/2026.................................91

**KIAMBATANISHO NAMBARI 5A:** Mafunzo ya Muda Mrefu.........97

**KIAMATANISHO NAMBARI 5B:** Mafunzo ya Muda Mfupi.........97

**KIAMBATANISHO NAMBARI 6A:** Huduma za Meli........................97

**KIAMBATANISHO NAMBARI 6B:** Huduma za Mizigo. ..................97

**KIAMBATANISHO NAMBARI 7A:** Idadi ya Abiria waliohudumiwa katika Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026.......................98

**KIAMBATANISHO NAMBARI 7B:** Idadi ya Ndege zilizohudumiwa katika Kipindi cha Julai 2025 Hadi Machi 2026 ............... ......98

**KIAMBATANISHO NAMBARI 7C:** Kampuni za Ndege zilizotumia Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.......................99

**KIAMBATANISHO NAMBARI 8:** Orodha ya Barabara zinazoendele na zitakazoanza ujenzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027........ ...103

**KIAMBATANISHO NAMBA 9:** Maeneo ambayo yatafanyiwa Maboresho kwa Kujenga Misingi /Mitaro ya Kuondoa Maji ya Mvua yanayotuama (Jumla ya Kilomita 78.05 ya Msingi/ Mitaro Itajengwa)..............................111

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lizingatie, lijadili na hatimae likae kama kamati ili liweze kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kazi za kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** Nianze kwa kumshukuru Allah (S.W) kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Mkutano wa Tatu (3) wa Baraza la Wawakilishi la 11 kinachojadili Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ikiwa leo hii tunajadili utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie hekima, utulivu na busara wakati wa kujadili hotuba ya bajeti ya Wizara ninayoiongoza kwa masilahi mapana ya ustawi wa Taifa letu.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Wananchi wa Zanzibar kwa mara nyengine katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 na kuingoza Zanzibar kwa kipindi cha Pili cha Awamu ya Nane ili kuendelea kuwaletea maendeleo zaidi wananchi wa Zanzibar. Kwa hakika Mheshimiwa Rais anaendelea kutekeleza kwa vitendo ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 - 2030. Kipekee tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kusimamia vyema suala la Amani, Utulivu na Mshikamano wa kitaifa na kuhakikisha kuwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 unafanyika kwa Amani na Utulivu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

5. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar; Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais amekuwa akimsadia sana Mheshimiwa Rais katika kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Barazani ambayo imeonesha dira na mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka ujao wa fedha. Pia, namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa miongozo anayotupatia katika Wizara yetu inayotuwezesha kutekeleza kazi zetu za Wizara kwa ufanisi na umakini.

6. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa kumteua Mheshimiwa Badria Atai Masoud kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Hivyo, tunao wajibu mkubwa wa kufanya kazi kwa bidii na uaminifu ili kukidhi matarajio yake kwa nchi hii ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za ujenzi na usafiri zilizo salama na zinazokidhi mahitaji.

7. **Mheshimiwa Spika,** Namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano yao makubwa wanayotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

8. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambalo umekuwa

ukiliongoza kwa hekima, busara na umahiri mkubwa. Aidha, pongezi hizi ziende pia kwa Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kusaidia kuendesha shughuli za Baraza hili.

9. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mapenzi makubwa sana natoa shukurani zangu kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi makini wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mihayo Juma N'hunga, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mwera, kwa uchambuzi wao makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Fungu 061) kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027 na kupitisha Bajeti ya Wizara. Ushauri, maoni na maelekezo yaliyotolewa na Wajumbe wa Kamati yamezingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027.

10. **Mheshimiwa Spika,** Ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuongoza Wizara mbalimbali wanazozisimamia. Ninawaahidi ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Serikali.

## B. MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA.

11. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ina jukumu la kusimamia Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na kuandaa na kusimamia Sera, Sheria, Miongozo na kuendeleza tafiti na ubunifu unaohusiana na Sekta hizo.

12. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inatekeleza majukumu hayo kupitia Idara (2), Ofisi kuu Pemba na

Taasisi kumi (10) zinazojitegemea. Idara hizo ni: - Idara ya Uendeshaji na Utumishi na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Taasisi zinazojitegemea ni:- Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Shirika la Bandari, Shirika la Meli, Wakala wa Barabara, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari, Wakala wa Majengo, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi pamoja na Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo.

## C. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA 2025/2026.

13. **Mheshimiwa Spika,** Wakati tunawasilisha Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi ilikuwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktaba, 2025. Mheshimiwa Rais aliunda Wizara mbili mpya kutoka iliyokuwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambazo ni Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, na Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu.

14. **Mheshimiwa Spika,** Hivyo, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi ilikuwa na vipaumbele vifuatavyo:-

   i. Miundombinu ya usafiri wa barabara ikiwemo kuendelea na ujenzi na matengenezo ya barabara kuu, barabara za mjini na barabara za ndani;

   ii. Kuendelea na utekelezaji wa mkakati wa kupunguza ajali barabarani ili kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuwapatia elimu ya usalama barabarani makundi tofauti ya jamii pamoja na kufanya ukaguzi wa barabarani ili kubaini wanaokiuka utaratibu.

   iii. Kuimarisha miundombinu ya bandari ikiwemo kuanza kwa ujenzi wa Bandari Jumuishi ya

Mangapwani, ujenzi wa Bandari ya Abiria na Mzigo Maruhubi, ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini, uimarishaji wa Bandari ya Mkoani na ujenzi wa Bandari Kavu Maruhubi;

iv. Kuendelea na ujenzi wa boti mbili za mwendo wa kasi ambazo zitafanya kazi ya kusafirisha abiria baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam.

v. Kuimarisha miundombinu ya usafiri wa anga kwa kuanza na kuendelea na ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba, ujenzi wa Jengo la Abiria (Terminal II) pamoja na kukamilika ujenzi wa Jengo la Abiria (Terminal 1) katika Uwanja wa AAKIA.

vi. Kuimarisha miundombinu ya kuondolea maji ya mvua ndani ya mji wa Zanzibar.

vii. Kuendelea kusimamia miradi mbali mbali ya ujenzi wa majengo ya Serikali kwa kutoa huduma za ushauri elekezi kwa miradi hiyo.

viii. Kuimarisha karakana za Serikali kupitia ubia na kampuni binafsi (PPP) ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma kwa kufanya matengenezo ya magari Unguja na Pemba.

ix. Kutayarisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali itakayowezesha kusimamia na kutoa huduma bora kwa jamii katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi.

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026

### D.1. Mapato yaliyokusanywa na Wizara kwa Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026

15. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 5,204,920,000** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 3,982,100,400.** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 2,006,988,171.7** zimekusanywa sawa na **asilimia 50.4** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 38.55** kwa makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho namba 1** kinatoa ufafanuzi.

**D.2. Fedha zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026**

16. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya mabadiliko ya Wizara, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilibaki na Programu kuu tatu (3) ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, zilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,511,578,178,515.** Kati ya fedha hizo **TZS 3,413,213,000** ni mshahara, **TZS 2,984,496,515** ni matumizi ya uendeshaji wa Ofisi, **TZS 31,766,900,000** ni Ruzuku na **TZS 1,473,413,569,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara ilipanga kutumia jumla ya **TZS 1,141,851,838,018.** Kati ya fedha hizo, **TZS 2,559,909,750** ni mshahara, **TZS 2,175,499,194** kazi za kawaida, **TZS 26,712,762,363** ruzuku na **TZS 1,110,403,666,711** kazi za maendeleo.

17. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi wa Machi, 2026 jumla ya **TZS 876,385,436,123.1** zimepatikana sawa na **asilimia 76.75** ya makadirio ya bajeti kwa kipindi cha miezi tisa na **asilimia 57.97** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **TZS 1,993,753,917.5** ni mshahara sawa na **asilimia 77.9** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 58.4** ya makadirio ya mwaka, **TZS 1,198,420,588** ni kazi za kawaida sawa na **asilimia 55.1** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 40.2** kwa mwaka, **TZS 14,424,090,537** ni Ruzuku kwa taasisi zilizomo ndani ya Wizara sawa na **asilimia 53.9** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 45.4** ya makadirio ya mwaka na **TZS 858,769,171,080.6** ni kwa kazi za maendeleo sawa na

**asilimia 77.3** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 58.28** ya mwaka. **Kiambatanisho namba 2A** na **2B** kinatoa ufafanuzi.

**D.3. Utekelezaji wa Malengo ya Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imetekeleza kazi zake kupitia Programu kuu tatu (3) na Programu ndogo tano (5). Utekelezaji wa malengo ya programu hizo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ni kama ifuatavyo: -

**PP0101- PROGRAMU YA USAFIRISHAJI.**

**19.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilikuwa na lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri ili ziwe bora, salama na endelevu na zitakazoleta matokeo bora katika sekta ya uchukuzi. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu ya Usafirishaji ilikuwa na Programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

**SP010101 - Programu Ndogo: Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.**

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari na Wakala wa Barabara Zanzibar. Kupitia taasisi hizi programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara hii iilipanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. Kuimarisha miundombinu ya Barabara Unguja na Pemba.

22. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha miundombinu ya barabara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ilipanga kujenga jumla ya kilomita 447.63 kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba, kati ya kilomita hizo, kilomita 200 ni barabara Kuu, kilomita 208.73 ni barabara za ndani na kilomita 38.9 ni Barabara za Mjini kupitia miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara.

23. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya kilomita 240.7 za barabara zimekamilika kwa kiwango cha lami; Ikiwa kilomita 105.1 barabara kuu, kilomita 54.6 barabara za Mjini, na kilomita 81 ni barabara za ndani na Vijijini. Ujenzi wa barabara hizi umetekelezwa kupitia miradi ifuatayo:-

**i. Matengenezo ya Barabara za Mjini.**

- **Ujenzi wa Barabara za Mjini Unguja zenye Urefu wa Kilomita 100.9:** Kwa kipindi cha Julai - Machi 2025/2026, jumla ya kilomita 36.742 zimekamilika kwa kiwango cha lami na kuufanya mradi huu kufikia jumla ya kilomita 98 zilizokamilika kwa kiwango cha lami. Pia mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara za juu (Flyover) katika eneo la Mwanakwerekwe Round About ambayo imekamilika, eneo la Amani ambayo inaendelea na ujenzi wa mtaro wenye urefu wa kilomita 2.6 katika eneo la Tomondo ambao upo katika hatua za mwisho kukamilika. Kwa ujumla mradi huu umefikia asilimia 86 ya utekelezaji. **Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika

**ii. Ujenzi wa Barabara za Vijijini na Ndani Unguja na Pemba.**

- Mradi huu una lenga kujenga barabara za Ndani zenye Urefu wa Kilomita 275.9 Unguja na Pemba:

Kwa kipindi cha Julai - Machi 2025/2026, jumla ya kilomita 65.4 zimekamilika kwa kiwango cha lami na kuufanya mradi huu kufikia jumla ya kilomita 213 (135.7 Unguja na 77.3 Pemba) zilizokamilika kwa kiwango cha lami. Mradi huu umefikia asilimia 95 ya utekelezaji. **Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika

- **Mradi wa Usanifu, Kuboresha na Kujenga Barabara Mlisho (Feeder Road 163.22 km):** Wizara inaendelea kuzifanyia usanifu, kuboresha na kuzijenga jumla ya Kilomita 163.2 barabara za Mlisho Unguja na Pemba katika kiwango cha lami. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 jumla ya kilomita 10.08 zimekamilika kwa kiwango cha lami, na kuufanya mradi huu kufikia asilimia 42.1 ya utekelezaji wa jumla. **Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika

**iii. Ujenzi wa Barabara Kuu Unguja na Pemba.**

- **Ujenzi wa Barabara ya Tunguu – Makunduchi km 48, Fumba – Kisauni km 12 na Mkoani – Chake 43.5.** Mradi upo katika hatua ya Mandalizi ya Awali (Design and Mobilization stage). Aidha, kazi za ujenzi wa kambi ya Mkandarasi katika eneo la Muyuni na Kibele unaeendelea na umefikia asilimia 90. Pia, Wizara inaendelea kufanya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Makaazi (Resseltment Action Plan - RAP) ili kuanza maandalizi ya ulipaji wa fidia.

- **Ujenzi wa Barabara ya Wete – Chake:** Jumla ya kilomita 22.1 za barabara ya Wete – Chake zimekamilika kwa kiwango cha lami. **Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika

- **Ujenzi wa Barabara Kuu kilomita 277 Unguja na Pemba:** Kwa kipindi cha Julai - Machi 2025/2026, jumla ya kilomita 10.6 zimekamilika kwa kiwango cha lami na kuufanya mradi huu kufikia jumla ya kilomita

17.8 zilizokamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, jumla ya kilomita 52.23 za barabara zinaendelea kwa hatua mbali mbali za ujenzi ikiwemo barabara za Mkwajuni – Kijini (kilomita 9.3), Unguja Ukuu – Uzi – Ng'ambwa (kilomita 8.7), Chanjamjawiri – Tundauwa (kilomita 10.75) na Chake chake – Wesha (kilomita 7.7) na Makubduchi – Mtende – Kizimkazi (kilomita 14). **Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika

- **Ujenzi wa Barabara Kilomita 65 Unguja na Pemba:** Wizara inaendelea na Usanifu, Uboreshaji na Ujenzi na Barabara zenye Urefu wa kilomita 65.5 za Unguja na Pemba. Kwa Mwaka 2025/2026 jumla ya kilomita 18 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Mradi umefikia asilimia 16 ya utekelezaji wa jumla. Kiambatanisho nambari 3A kinahusika

- **Ujenzi wa barabara zinazounganisha eneo la Mangapwani na nyenginezo zenye urefu wa kilomita 113.8:** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya kilomita 67.6 zimekamilika kwa kiwango cha lami na kuufanya mradi huu kufikia jumla ya kilomita 74.4 zilizokamilika kwa kiwango cha lami. Pia mradi huu ulijumuisha ujenzi wa Daraja la Pangatupu lenye urefu wa mita 100 ambalo limekamilika. Kiujumla mradi huu umefikia asilimia 78 ya utekelezaji wa jumla**. Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika.

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Orodha ya barabara zilizokamilika kwa kiwango cha lami kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 kwa mgawanyo wa kila Mkoa inaonekana katika **Kiambatanisho nambari 3B.**

iv. **Uwekaji wa Kamera za kisasa za kusimamia Usafiri wa Barabarani (Smart Traffic Camera).** Katika kuimarisha usalama kwa watumiaji wa barabara pamoja na kubaini makosa yanayotokana na uvunjifu wa sheria na

kanuni za usalama barabarani, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imeshasaini Mkataba na Muwekezaji, Zenj General Marchandise kwa ajili ya zoezi hili. Kwa sasa, kazi imeanza kwa kuweka kamera ya majaribio katika eneo la Dole na kamera 14 kwa ajili ya maeneo mengine zimeshafika Zanzibar. Miongoni mwa maeneo ambayo yatafungwa kamera hizo ni Mazizini, Kiembesamaki, Baraza la Wawakilishi, Maisara, Mnazi Mmoja, Mombasa Sokoni, Msumbiji, Darajabovu na Kilimani.

v. **Kuimarisha mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar.** Wizara ilipanga kukamilisha utafiti wa kuimarisha mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar unatekelezwa na Mshauri Elekezi, Kampuni ya IDOM Consulting, Engineering, Architecture ya Hispania kupitia Ruzuku kutoka Serikali ya Hispania. Utafiti huu umekamilika na umetoa mapendekezo ya namna ya kuimarisha mfumo wa kisasa wa usafiri wa umma Zanzibar, ikiwemo marekebisho Sera na Kanuni, Matumizi ya teknolojia kama vile ununuzi wa tiketi, uwekaji wa alama za usalama barabarani, Ujenzi wa vituo vya mabasi, ujenzi wa maeneo maalamu ya kuchaji magari ya umeme, kutoa elimu ya usalama barabarani kwa jamii pamoja na kupendekeza kuwepo kwa ruti aina mbali mbali ambazo zitaunganisha usafiri wa mjini.

**b. Uimarishaji wa Miundombinu ya Usafiri wa Anga Unguja na Pemba.**

**25.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara katika kuimarisha miundombinu ya Usafiri wa Anga, kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na huduma za Usafirishaji ilipanga kuendelea na Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, kukamilisha ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II Kwamu ya kwanza, kuanza kwa Awamu ya Pili ya Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II, ujenzi wa

maegesho ya ndege (Apron) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa wa AAKIA na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi.

**26.** **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i. **Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba:** Serikali imepanga kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuongeza urefu wa barabara ya kutua na kurukia ndege (runway and taxi way) kutoka kilomita 1.5 hadi kufikia kilomita 2.51, kujenga Jengo Jipya la Abiria (Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800) na zinazolingana. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Pemba Airport Construction Consortium (PROPAV Infrastructures) kwa mkopo kutoka "United Kingdom Export Finance (UKEF)" wenye gharama ya Euro 170,000,000 sawa na TZS 467,659,800,000. Kazi za ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba ilianza rasmi Oktoba, 2025. Kazi inayoendelea ni ujenzi wa njia ya kutua na kuruka ndege (Runway) kwa upande wa Kaskazini (North). Hadi kufikia Machi, 2026 mradi huu umefikia asilimia 3.6 ya utekelezaji.

ii. **Ujenzi wa Jengo jipya la Pili la Abiria (Terminal II) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume:** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imefanikiwa kuendelea na Ujenzi wa Jengo Jipya la Pili la Abiria (Terminal II) na hadi kufikia Machi, 2026 ujenzi wa jengo hili umefikia asilimia 85. Jengo hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 1,300,000 kwa mwaka.
Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeanza ujenzi wa daraja (bridge) linalounganisha Jengo Jipya la Abria TB2 na Jengo la TB 3 ili kuunganisha huduma baina ya majengo hayo. Daraja hilo litakuwa

na ukubwa wa mita za mraba 7,000, ambalo litajumuisha eneo la kuondokea abiria, maeneo ya biashara pamoja na sehemu ya kukaa abiria kwa ajili ya kusubiri ndege. Kwa ujumla Daraja litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 600,000 kwa mwaka.

iii. **Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi:** Wizara ilipanga kuanza ujenzi wa uwanja wa ndege wa Nungwi ili uweze kutoa huduma kulingana na viwango vya kimataifa. Serikali imeshaingia mkataba ya Kampuni ya INTEXT kwa ajili ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi ambao utakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa za aina ya Code E. Kwa sasa Serikali inakamilisha tathmini ya ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

iv. **Ujenzi wa maegesho ya Ndege (Apron) katika Uwanja wa AAKIA:** Mradi huu unahusisha upanuzi wa magesho ya ndege yaliyopo sasa kwa kujenga maegesho mpya ya ndege yenye uwezo wa kuegesha ndege zenye ukubwa wa Code C (3) na Code E (2) au ndege ndogo na za kati zaidi ya 15. Ujenzi umeanza na kazi zilizofanyika ni kukamilisha kazi ya usafishaji wa eneo la ujenzi, kuendelea na uwekaji wa kifusi (subgrade) pamoja na ujenzi wa mitaro ya kupitisha maji. Hadi kufikia Machi, 2026 mradi huu ulifikia asilimia 20 ya utekelezaji.

### iii. Miundombinu ya Usafiri wa Baharini

27. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara katika kuimarisha miundombinu ya Usafiri wa Baharini, kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na huduma za Usafirishaji ilipanga kuendelea na ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani, kukamilisha nyumba za fidia katika eneo la Mangapwani pamoja na kujenga Bandari mpya ya kisasa ya Abiria katika eneo la Maruhubi. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i. **Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani.** Ujenzi wa bandari hii unaendelea na kazi zilizofanyika kwa kipindi cha miezi tisa ni kukamilisha usafi wa eneo la mradi, kukamilisha tafiti zote za usanifu wa bandari ikiwemo uchambuzi wa udongo, usanifu wa kina wa bandari, kina cha maji, mawimbi na upepo. Aidha, ujenzi wa kiwanda cha zege kwa ajili ya kuchakata malighafi za zege pamoja na kiwanda cha kutengeneza vyuma unaendelea. Kwa sasa Mkandarasi anaendelea na kazi ya uchimbaji wa udongo katika sehemu ya kuwekea makontena. Kwa ujumla mradi hu umefikia asilimia 14 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2028.

ii. **Ujenzi wa Nyumba za Fidia eneo la Mangapwani.** Hadi kufikia Machi, 2026 Wizara imefanikiwa kukamisha ujenzi wa nyumba zote 370 zilizopangwa kujengwa katika eneolaBumbwiniikiwanifidiakwawananchiwalioathirika na Ujenzi wa Bandari Jumuishi Mangapwani. Kwa sasa Wizara imepanga kufanya uhakiki wa kuwatambua wananchi wanaohitaji nyumba ili wapatiwe na wale wanahitaji fedha, walipwe fedha.

iii. **Ujenzi wa Bandari ya Abiria (Passanger Ferry Terminal - Maruhubi):** Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano na ZF Devco na utajumuisha Baji kwa meli za mwendokasi, kituo cha kuegesha vyombo vya RoRo, jengo jipya la kituo cha abiria, maghala, eneo maalum la kiuchumi lenye huduma za burudani na malazi, vituo vya biashara vya B2B, kituo cha ndege za baharini, kituo cha mabasi, na vituo vya biashara. Mradi unatekelezwa kwa awamu tatu ndani ya kipindi cha mkataba wa ukodishaji. Ujenzi wa bandari ya Maruhubi unaendelea kwa hatua mbalimbaili ikiwemo kukamilika kwa ujenzi wa Daraja na Baji kwa asilimia 100. Aidha, kazi za ujazaji wa kifusi, ushindiliaji wa eneo la ujenzi, ujenzi wa ghala, sehemu ya maegesho ya magari, ujenzi wa ghala la Forodha, ujenzi wa Majengo madogo madogo, ujenzi

wa barabara na ujenzi wa mizani ya kupimia mizigo unaendelea. Vilevile, majaribo ya ufungaji wa meli ya aina za Ro Ro katika bandari hiyo yamefanyika.

28. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,063,413,569,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 770,040,959,452.6** zimepatikana sawa na **asilimia 72.41** ya makadirio ya bajeti.

## WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

29. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu ndogo ya Usimamzi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kuimarisha mtandao wa barabara Zanzibar kwa kuzijenga na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika kwa usalama muda wote. Aidha, Wakala wa Barabara Zanzibar inatoa huduma za Usimamizi na Ushauri wa Kitaalamu kwa Wakandarasi wanaojenga barabara Zanzibar.

30. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Barabara Zanzibar kwa Kipindi cha Julai, 2025 – Machi 2026, imetekeleza kazi kama ifuatavyo:-

    a. **Ujenzi wa Barabara.** Wakala wa barabara inaendelea na ujenzi wa barabara mbalimbli kwa tabaka tofauti za kifusi. Barabara hizo ni:- Mchangani - Msikitini zenye urefu kilomita 1.3 ambayo imefikia asilimia 80, barabara ya ndani ya Uchukuni yenye urefu wa kilomita 4.5 ambayo imefikia asimilia 29 na barabara ya Pandani – Mlindo yenye urefu wa kilomita 3.2. ambayo imefikia asilimia 43.

b. **Matengenezo ya Barabara.** Kwa upande wa matengenezo ya barabara, Wakala wa Barabara Zanzibar ilipanga kuziba mashimo kwa barabara za lami kwa maeneo yenye mita za mraba 4,000 kwa upande wa Unguja na mita za mraba 4,500 kwa upande wa Pemba. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya mita za mraba 2,834 za mashimo yamezibwa sawa na asilimia 70.9 kwa Unguja na jumla ya mita za mraba 2,040 za mashimo yamezibwa sawa na asilimia 45.3 kwa Pemba. Maeneo yaliyofanyiwa kazi kwa Unguja ni:- barabara ya Kinyasini - Kilombero, Kipandoni – Kiwengwa, Mshelishelini – Pwani Mchangani, Mahonda - Donge - Mkokotoni, Michenzani – Maisara. Kwa upande wa Pemba maeneo yaliyofanyiwa kazi ni :- Barabara ya Chanjaani – Uwanja wa Ndege, Chanjaani - Chake, Melitano - Madenjani, Kilindini - Konde, Chake – Wesha na Ole – Kengeja.

c. **Matengenezo ya Dharura ya barabara za Unguja na Pemba:** Wakala ilifanikiwa kufanya matengenezo ya dharura barabara za Unguja kwa kujenga kituo cha daladala eneo la Jamuhuri Garden mita 75, kujenga kwa kifusi barabara za Kianga- Flower mita 400, Mshelishelini Mambo sasa - Msikitini mita 150, Kisauni - Mkunazi Samaki – Jambonia mita 600, Kikungwi Skuli - Kijijini mita 500, Chuo cha Mafunzo - Hanyengwa Mchana mita 800 na Ofisi ya Usalama - Mwera mita za 450. Kwa upande wa Pemba Wakala ilifanikiwa kuifanyia matengenezo ya dharura barabara mchepuko yenye urefu wa mita 100 iliyopo eneo la Mfikiwa njia ya kuelekea Uwanja wa Ndege kwa kuweka lami.

d. **Uwekaji wa Alama na Michoro Barabarani kwa Unguja na Pemba.** Wakala wa Barabara imefanikiwa kukamilisha kazi ya uwekaji wa alama na michoro kwa barabara ya Paje - Makunduchi yenye urefu wa kilomita 18 kwa asilimia 90 na Uwekaji wa alama ya vivuko

(Zebra Crossing) pamoja na kuweka alama za usalama katika maeneo yaliyowekwa matuta ya barabara ya Mzambarau Takao – Mzambarau Karim.

e. **Utunzaji wa Barabara.** Katika kuendeleza programu ya utunzaji wa barabara, Wakala wa Barabara kwa kipindi cha Julai, 2025 - Machi 2026 ilipanga kufanya usafi wa madaraja, misingi na kukata majani barabara zenye urefu wa kilomita 33.9 kwa Unguja na kilomita 213.5 kwa Pemba. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya kilomita 30.9 kwa Unguja na kilomita 72 kwa Pemba zilifanyiwa usafi kwa kukatwa majani ikiwa ni sawa na asilimia 91.2 Unguja na asiilimia 33.7 Pemba.

f. **Ushauri Elekezi.** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wakala wa barabara imesimamia ujenzi wa njia za watembea kwa miguu na uwekaji wa Taa barabarani kwa barabara za Kizimkazi, Ujenzi wa barabara ya Mbuzini - Selemu (Mwakaje) ambazo zilijengwa na Kampuni ya Ecocity. Kwa upande wa Pemba, Wakala ilisimamia ujenzi wa barabara ya Mgelema - Wambaa (km 4.1), Wambaa - Msiwakwe (km 0.35), Wete - Hospitali ya Wilaya Kinyasini (km 0.7) kwa kiwango cha zege. Barabara hizi zimejengwa na Kampuni ya OCRA Construction Limited.

g. **Kuratibu na Kusimamia shughuli za Uendeshaji wa Afisi ya Wakala**

Wakala iliweza kusimamia shughuli za kawaida ikiwemo, matengenezo madogo madogo ya Afisi, upatikanaji wa Huduma za Umeme, Maji na Stahiki za Watumishi kwa Unguja na Pemba.

**Matumizi ya Wakala wa Barabara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**.

**31.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu ndogo

ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 25,853,200**,000 ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya mishahara, kazi za kawaida na matengenezo ya barabara Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo, **TZS 6,240,000,000** ni mishahara, **TZS 968,774,000** ni matumizi mengineyo na **TZS 18,644,426,000** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

32. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS 11,251,734,213.5** zimetumika sawa na **asilimia 43.52** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TZS 3,483,833,151.5** ni mshahara, **TZS 262,486,085** ni matumizi mengineyo na **TZS 7,505,414,977** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara Unguja na Pemba.

**WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR**

33. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepewa jukumu la kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto vya Serikali na binafsi kupitia Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba pamoja na kutoa ushauri wa kitalaamu juu ununuzi na uuzaji wa vyombo vya moto vya Serikali.

34. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

a. **Matengenezo ya Vyombo vya Moto (Gari) vya Serikali na Binafsi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipanga kufanya matengenezo ya vyombo vya moto 2,700 vya Serikali na Binafsi kwa Unguja na Pemba na hadi kufikia Machi 2026, imefanikiwa kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto 1,508 sawa asilimia 55.8 ya makadirio ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Kati ya vyombo hivyo, vyombo vya moto 1,458 ni vya Serikali na 50 ni vya watu

binafsi. Aidha, jumla ya vyombo 1,264 vimefanyiwa matengenezo Unguja na vyombo 194 zimefanyiwa matengenezo Pemba.

b. **Utoaji wa Ushauri wa Kitaalamu Juu ya Ununuzi na Uuzaji wa Vyombo vya Moto vya Serikali:** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wakala imefanikiwa kutoa ushauri wa Kitaalamu kwa taasisi 15 (11 ununuzi na 4 uuzaji). Wakala ilishiriki katika kufanya ukaguzi wa vyombo vilivyonunuliwa na vilivyouzwa kwa Taasisi za OR-TAMISEMI, ZAFICO, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Afisi ya Rais - Fedha na Mipango, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Kikosi cha Zima Moto na Uokozi pamoja na Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali.

c. **Uimarishaji wa Ofisi na Karakana Unguja na Pemba:** Katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za Kiutawala na Kiufundi kwa wakati na kuhakikisha upatikanaji wa huduma hizo muda wote wa kazi, Wakala imefanikiwa kukodi jengo kwa ajili ya huduma za ofisi katika maeneo ya Mchina Mwanzo kwa Unguja pamoja na kuipatia vifaa vya kutendea kazi vikiwemo vifaa vya kuandikia (stationaries), upatikanaji wa huduma ya maji na umeme, vifaa vya kufanyia usafi, mafuta, matengenezo ya vyombo vya usafiri vya Wakala, vipuri na vilainishaji pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mtandao katika mfumo wa HR kwa ajili ya kazi za Ofisi.

d. **Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi.** Wakala ilipanga kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi 19 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2026, imefanikiwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi 15 sawa na asilimia 78.9 ya wafanyakazi waliopangiwa kupatiwa mafunzo kwa kipindi hicho. Kati ya wafanyakazi hao, 4 wamepatiwa mafunzo ya muda

mrefu na wafanyakazi 11 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi Unguja na Pemba (Unguja, 9 na Pemba, 2).

**Mapato na Matumizi**

35. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 435,000,000** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wakala ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 328,325,000** (Unguja **TZS 302,100,000** na Pemba **TZS 26,225,000**) na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2026, jumla ya **TZS 13,328,889** (Unguja **TZS 10,592,164** na Pemba **TZS 2,736,725**) zilikusanywa sawa na **asilimia 4** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 3** ya makadirio ya mwaka.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipanga kutumia jumla ya **TZS 2,873,000,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 1,531,800,000** ni mshahara na **TZS 1,341,200,000** ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 1,415,507,012.5** zimepatikana sawa na **asilimia 49.26** ya makadirio ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Kati ya fedha, jumla ya **TZS 982,285,236.5** ni mshahara na **TZS 433,221,776** ni matumizi mengineyo (Unguja **TZS 296,567,276** na Pemba **TZS 136,654,500**).

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,092,298,979,000** kwa kazi za kawaida, ruzuku na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia programu hii. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2026 jumla ya **TZS 782,708,200,678.6** zimetumika sawa na **asilimia 71.7** ya makadirio ya mwaka.

**PP0105 - PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO.**

**38.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara katika kazi za ujenzi na majengo ya Serikali na binafsi yaliyo salama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa miongozo iliyopo na yenye kukidhi mahitaji ya watumiaji wote. Programu hii ina programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.

**SP010501 - Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.**

**39.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Wakala wa Majengo Zanzibar na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara wa ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyo salama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa Sheria na miongozo iliyopo.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

**40.** **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilipanga kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Mitaro ya Maji ya Mvua katika mji wa Zanzibar pamoja na mradi wa kuimarisha miundombinu mbalimbali itakayosaidia kukuza Uchumi katika miji ya Unguja na Pemba (BIG - Z). Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

a. **Ujenzi wa Misingi/mitaro ya Kondolea Maji ya Mvua.** Wizara tayari imeshatia Saini mkataba wa ujenzi wa misingi ya kuondoa maji ya mvua katika maeneo 28 ya Unguja ambayo yana changamoto ya kupata mafuriko wakati wa mvua katika maeneo ya mji wa Zanzibar. Aidha, ujenzi wa msingi wa maji wenye urefu wa kilomita 2 pamoja na kipande cha barabara yenye urefu wa mita 400 katika eneo la Soko la Chuini (Kwa nyanya) umefikia asilimia 90.

b. **Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG - Z).** Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu itakayosaidia kukuza Uchumi katika miji mbalimbali Unguja na Pemba ikiwemo mji wa Mkoani, Chake Chake, Wete na Micheweni kwa upande wa Pemba na Maeneo ya Sebleni – Kwa wazee, Jang'ombe na Magomeni kwa upande wa Unguja.

Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara katika kuimarisha miundombinu na uboreshaji wa Maeneo katika mji wa Unguja imefanikiwa kujenga jumla ya kilomita 10.2 za barabara kupitia mradi huu wa BIG - Z. **Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika. Miongoni mwa kazi zilizofanyika ni; ujenzi wa barabara ya Jang'ombe, barabara ya Sogea - Denja, barabara ya Mosi, Gongo store kwa wazee, Msumbiji kwa Mpechi, Sebleni, Wawi bekari, Wandaras – Makada pamoja na kuendelea kwa ujenzi wa barabara ya Felix Moumie kwa hatua mbali mbali.

Kwa upande wa Pemba, Wizara imetiliana saini Mkataba na Kampuni ya Gopa kutoka Dar es Salaam tarehe 16 Februari 2026 kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu muhimu ikiwemo barabara, masoko, vituo vya mabasi, njia za waenda kwa miguu, mitaro ya maji ya mvua pamoja na ukarabati wa jengo la Old Fort (Makumbusho) liliopo Mji wa Chake Chake ikiwa na lengo la kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Kazi za ujenzi zilianza ndani ya mwezi wa Mei, 2026.

41. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 410,150,730,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi na kazi za kawaida zilizo chini ya Programu hii. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 88,781,611,628** zimetumika sawa na **asilimia 21.64** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TZS 6,560,130,934** zinatoka SMZ, **TZS 82,168,080,694**

zinatoka kwa Mfadhili (Benki ya Dunia) kwa ajili ya Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumishi Zanzibar na **TZS 53,400,000** ni kwa kazi za kawaida.

**WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR**

42. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo ilianzishwa kupitia Tangazo la Kisheria Nambari 50 la tarehe 12 Mei, 2017. Taasisi hii ina jukumu la kuendeleza majengo ya Serikali, kujenga, kukodisha na kukopesha Majengo ya Serikali kwa bei nafuu kwa watumishi wa umma wanaostahiki, kuandaa na kuweka utaratibu mzuri wa kumiliki makaazi kwa watumishi wa umma, kutoa huduma za Ushauri wa Ujenzi, kusimamia Majengo ya Serikali pamoja na kupanga ujenzi wa Majengo ya Serikali kulingana na mahitaji.

43. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wakala wa Majengo Zanzibar imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

a. **Kuandaa Nyaraka za Ujenzi.** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Majengo ilipanga kuandaa nyaraka za ujenzi 39 na hadi kufikia Machi, 2026, imefanikiwa kuandaa nyaraka 10 za ujenzi (Ramani na Gharama) sawa na asilimia 26 ya makadirio ya mwaka. Kati ya nyaraka hizo, 5 zimeandaliwa Unguja na 5 zimeandaliwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 4A** kinahusika.

b. **Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi.** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Majengo ilipanga kusimamia miradi ya ujenzi 47 na hadi Machi, 2026, imefanikiwa kusimamia miradi ya ujenzi 42 (Construction Supervision) sawa na asilimia 89. Kati ya miradi hiyo 32 imesimamiwa Unguja na 10 imesimamiwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 4B** kinahusika.

**Mapato na Matumizi**

**44.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026, Wakala ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 2,165,000,000** kutoka katika vianzio vyake (**TZS 1,800,000,000** Unguja na **TZS 365,000,000** Pemba). Hadi kufikia Machi, 2025, imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS 297,797,608.7** (Unguja ni **TZS 269,427,608.70** na Pemba ni **TZS 28,370,000**) sawa na **asilimia 14** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Kwa mwaka 2025/2026, Wakala wa Majengo ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 3,040,700,000** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 975,000,000** ni matumizi mengineyo na **TZS 2,065,700,000** ni ruzuku ya mshahara. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2026, jumla ya **TZS 1,756,849,311** zimetumika sawa na **asilimia 58** ya makadirio ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo, **TZS 289,681,450** ni matumizi mengineyo na **TZS 1,467,167,861** ni ruzuku ya mshahara.

**45.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo ilipangiwa kutumia Jumla ya **TZS 413,191,430,000** kwa kazi za kawaida, Ruzuku na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia programu hii. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2026 jumla ya **TZS 90,538,460,939** zimetumika sawa na **asilimia 21.91** ya makadirio ya mwaka.

**PP0104-UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

**46.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilikuwa na lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni:- Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti pamoja na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

**SP010401- Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji**

47. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu. Utekelezaji wa programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -

**IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

48. **Mheshimiwa Spika,** Idara hii imepewa jukumu la kusimamia na kutathmini shughuli za uendeshaji wa Wizara na kushughulikia maslahi pamoja na nidhamu kwa wafanyakazi. Aidha, Idara inaandaa na kusimamia mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa Wizara pamoja na utunzaji wa kumbukumbu na mali za Wizara. Idara pia, inajukumu la kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa wakati. Vilevile, Idara inatoa huduma za ununuzi na usimamizi wa mapato na matumizi ya Wizara.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipanga kuendelea kusimamia masuala ya kiutumishi na uendeshaji wa Wizara ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi na kuwapatia vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa kazi, kutoa makala na machapisho mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli na mafanikio ya Wizara pamoja na kuwajengea uwezo watendaji ili kuongezea ujuzi, ufanisi na tija kwa wafanyakazi wa Wizara wa Unguja na Pemba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa mujibu wa mpango wa mafunzo wa Wizara.

50. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kufanya matengenezo ya Ofisi, kununua vifaa mbalimbali vya Ofisi, kuvifanyia matenegenezo vyombo vya usafiri pamoja na

kuwapatia wafanyakazi stahiki zao ikiwemo malipo ya mishahara, malipo ya likizo pamoja na malipo baada ya saa za kazi.

Aidha, Idara imefanikiwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi kumi na nne (14) Unguja na Pemba. Kati ya hao, wafanyakazi kumi na moja (11) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi tofauti katika Vyuo vya ndani na Nje ya Unguja na Pemba na wafanyakazi tatu (3) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi Unguja na Pemba katika kozi tofauti. **Kiambatanisho nambari 5A** na **5B** kinahusika.

51. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 3,986,702,196** kwa kazi za kawaida, ikiwa **TZS 2,313,128,000** ni mishahara na **TZS 1,673,574,196** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS 1,736,687,443** zimetumika sawa na **asilimia 43.56** ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, **TZS 985,343,991** ni mishahara na **TZS 751,343,452** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**SP010402 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara**

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera mbali mbali katika sekta ya Ujenzi na Uchukuzi zinatayarishwa pamoja na kufuatilia utekelezaji wake.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

53. **Mheshimiwa Spika,** Idara hii imepewa jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera na Mipango ya sekta za Ujenzi na Uchukuzi. Aidha, Idara inaratibu kazi zote za maendeleo ya Wizara ikiwemo

kubuni, kutayarisha na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Pia, Idara inajukumu la kubuni na kufanya tafiti za kisekta ikiwemo ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.

**54.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipanga kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kutayarisha muongozo wa ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa kazi za Wizara, kutoa mafunzo ya utayarishaji wa bajeti kwa watendaji wa Wizara, kuratibu na kufanya tafiti zinazohusu Sekta za Wizara ikishirikiana na taasisi zilizochini ya Wizara. Kufanya mapitio Sera ya Usafiri Zanzibar ili iendane sambamba na mabadiko ya wakati, kuendelea kukusanya takwimu za Wizara, kuratibu na kuandaa vikao vya mashirikiano baina (SMZ) na (SJMT) pamoja na kuratibu na kusimamia mashirikiano ya kisekta, Kikanda na Kimataifa.

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. Idara imefanikiwa kuendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara, kutayarisha ripoti mbalimbali za utekelezaji wa kazi za Wizara pamoja na kukusanya takwimu zinazohusu sekta zinazosimamiwa na Wizara.

b. Idara imeanza maandalizi ya kutafuta Mshauri Elekezi kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sera ya Usafiri pamoja na Mpango Mkuu wa Usafiri (Transport Master Plan).

c. Idara imefanikiwa kuratibu shughuli mbalimbali zinazohusu Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi ikiwemo kushiriki mikutano mbalimbali inayajadili maendeleo ya Sekta hizo.

d. Idara imefanikiwa kuendelea kuratibu Taasisi na Mashirika mbalimbali yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na kuratibu na kushiriki katika vikao vya Mashirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi na uchukuzi Zanzibar na Wizara ya Uchukuzi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuimarisha mashirikiano pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya ujenzi.

e. Wizara imeanza maandalizi ya uazishwaji wa Kampuni ya Ndege Zanzibar kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina. Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu kuhusu uanzishwaji wa mfumo wa usafiri wa reli hapa Zanzibar.

f. Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaendelea kuratibu na kutayarisha Sheria mbalimbali za baadhi ya taasisi zilizomo katika Sekta ya Ujenzi na Usafiri ikiwemo Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Majengo, Sheria ya Karakana, Sheria ya Wakala wa Barabara, marekebisho ya Sheria zinazosimamia Bodi ya Usajili wa Wakandari na Bodi ya Wataalamu wa Ujenzi pamoja na Marekebisho Sheria Namba 5 ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006. Sheria zote hizi ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**56.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 971,723,000** kwa kazi za kawaida, ikiwa **TZS 506,958,000** ni mshahara na **TZS 464,765,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS 775,197,275** zimetumika sawa na **asilimia 79.8** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TZS 525,987,275** ni mshahara na **TZS 249,210,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**SP010403 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.**

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara kwa upende wa Pemba yanaratibiwa na kutekelezwa ipasavyo.

**OFISI KUU – PEMBA**

58. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu – Pemba kupitia Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba imepewa jukumu la kuratibu na kusimamia kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kuteketekeleza yafuatayo:-

a. Imeratibu na kusimamia maslahi ya wafanyakazi pamoja na kutoa huduma mbali mbali za Ofisi kwa lengo la kuweka mazingira bora ya kiutendaji. Huduma zilizotolewa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya likizo kwa watumishi, malipo baada ya saa za kazi, malipo ya safari kikazi, mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi, kulipia huduma za uendeshaji wa Ofisi pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya Jengo la Ofisi lililopo Tibirinzi Chake Chake Pemba.

b. Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya Ujenzi wa barabara, Uwanja wa Ndege na bandari kwa upande wa Pemba.

59. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi Kuu Pemba kupitia Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,129,344,319** kwa kazi za kawaida, ikiwa **TZS 593,127,000** ni mshahara na **TZS 536,217,319** ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS 626,889,787.5**

zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na **asilimia 55.5** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **TZS 325,948,772.5** ni mishahara na **TZS. 300,941,015** ni matumizi mengineyo.

## E. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULA 2025 HADI MACHI, 2026 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyoeleza hapo awali kuwa, Wizara ina Taasisi kumi (10) zinazojitegemea. Kati ya taasisi hizo, taasisi tatu (3) zinapata ruzuku kutoka Serikalini, Taasisi hizo ni Wakala wa Barabara, Wakala wa Majengo na Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari, maelezo ya utekelezaji wa taasisi hizi pamoja na malengo yake yameelezwa kwenye Programu za Wizara.

**61.** **Mheshimiwa Spika,** Taasisi saba (7) zinazojitegemea kibajeti kupitia mapato wanayokusanya, matumizi yake huidhinishwa na Bodi za Taasisi husika. Taasisi hizo ni:- Shirika la Bandari, Shirika la Meli, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi. Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 na malengo yanayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ni kama ifuatavyo: -

### E.1. SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR

**62.** **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari limepewa jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vya abiria na vyengine vya usafiri wa baharini.

**Utekelezaji wa kazi za Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.**

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Shirika la Bandari limefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. **Huduma za Bandari:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika lilipanga kuhudumia vyombo mbali mbali vya mizigo na abiria kwa kushirikiana na Waendeshaji Binafsi katika bandari zake za Unguja na Pemba. Shirika lilipanga kuhudumia safari za meli za kigeni 251 kwa mwaka na hadi Machi, 2026 jumla ya safari za meli za kigeni 292 zenye uzito wa GRT 1,943,640 zilihudumiwa sawa na asilimia 116 ya makadirio kwa mwaka.

Kwa upande wa safari za Meli za ndani, Shirika lilikadiria kuhudumia meli za ndani 11,000 kwa mwaka na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya safari za meli za ndani 5,218 zilihudumiwa sawa na asilimia 47 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Shirika lilikadiria kuhudumia safari za majahazi 9,500 kwa mwaka na hadi Machi, 2026 jumla ya safari za majahazi 9,027 zimehudumiwa sawa na asilimia 95 ya makadirio kwa mwaka, **Kiambatanisho nambari 6A** kinahusika.

Kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika lilipanga kuhudumia tani 1,700,000 za mizigo mchanganyiko kwa mwaka na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya Tani 1,452,664.88 za mizigo zimehudumiwa sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka. Pia, Shirika lilipanga kuhudumia mzigo wa majahazi tani 785,000 kwa mwaka na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya limehudumia Tani 945,896.19 za mizigo wa majahazi zilihudumiwa sawa na asilimia 120 ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa Mizigo ya Makontena, Shirika lilipanga kuhudumia Makontena 105,000 kwa mwaka na

hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya Makontena 73,450 yalihudumiwa sawa na asilimia 70 ya makadirio. Makontena hayo yamehudumiwa katika bandari ya Malindi, Fumba, Mkoani na Wete.

Aidha, Shirika lilipanga kuhudumia Mafuta ya kuwasha (Petroleum Fuel) lita 286,268,380 kwa mwaka na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya Mafuta ya kuwasha lita 242,763,148 zilihudumiwa sawa na asilimia 85 ya makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho namba 6B** kinahusika.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**64.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026, Shirika la Bandari limefanikiwa kutekeleza miradi ifuatayo:-

a. **Ujenzi wa Bandari ya Shumba:** Shirika la Bandari linaendelea na ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini itakayohudumia abiria na mizigo pamoja na kuhudumia meli zenye uzito wa Tani 2,000. Mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza inajumuisha ujenzi wa gati yenye urefu mita 45 na upana 20 na kazi hiyo inatekelezwa na Mkandarasi Comfix Engineering kwa gharama ya TZS 5,772,506,880.00. Hadi kufikia Machi, 2026, kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa gati, kuweka nguzo za kufunga kamba ya meli (bollard) na kinga za ukuta wa meli (fender). Hatua inayoendelea kwa sasa ni kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme. Utekelezaji wa mradi huu kwa awamu ya kwanza umefikia asilimia 92. Hadi kufikia Machi 2026, Mkandarasi ameshalipwa TZS. 5,145,948,889.35 sawa na asilimia 89 ya gharama za mradi.
Awamu ya Pili ya mradi huu inajumuisha ujenzi wa jengo la abiria, msikiti, maegesho (parking) ya vyombo vya moto na ukuta (uzio) unaozunguka eneo la bandari. Hadi kufikia Machi, 2026 kwa ujumla mradi huu umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Awamu ya Pili

hadi kukamilika kwake inatarajiwa kutumia jumla ya TZS 11,656,329,930.50 na hadi hadi kufikia Machi 2026 jumla TZS 5,306,935,033.95 zimetumika sawa na asilimia 46.

b. **Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani:** Shirika la Bandari inaendelea na maboresho ya Bandari ya Mkoani ambayo ipo chini ya Fumba Port kwa kuanza na ujenzi wa jengo la abiria, ofisi, maghala (warehouse) na utanuzi wa bandari kavu ambapo itakamilika ndani ya miezi 18 kwa gharama za TZS 7,428,260,623. Kwa ujumla, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 73 ya kazi zote zilizopangwa na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya TZS 3,094,108,336.12 zimetumika sawa na asilimia 41.65 ya gharama za mradi mzima. Pia, kumenunuliwa vifaa vya uchukuzi ili kuongeza ufanisi ambapo vifaa hivyo ni Reach staker, Terminal Tractor (TT) 3 na fork lift 2.

c. **Ujenzi wa Gati katika Bandari ya Fumba:** Mradi wa ujenzi wa gati katika Bandari ya Fumba ni muendelezo wa marekebisho katika bandari hiyo ili kuweza kuhudumia meli za makontena muda wote. Gati hiyo itakuwa na urefu wa mita 188 kutoka nchi kavu, urefu wa gati (kichwa cha gati) ni mita 350 na upana wa mita 48, na kina cha maji kitakuwa mita 13 wakati wa maji ya chini. Itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli mbili zenye uzito wa 50,000 DWT. Hadi kufikia Machi, 2026 kazi zilizofanyika ni kukamilisha michoro ya ujenzi wa gati, ujenzi wa crane platform pamoja na ujenzi wa jengo la utawala. Mradi huu umefikia asilimia 38 ya utekelezaji. Aidha, katika kuhakikisha bandari hii inatoa huduma kwa ufanisi kumenunuliwa vifaa vya mbali mbali ikiwemo Reach staker 3, Terminal tractor (TT) 5, fork lift 2, Mobile crane 2, Pilling barge 1, Crane barge 2, Work boat 1, tug boat 1, Dredger 2 na empty handler 2. Ujenzi wa Bandari hii unatarajiwa kugharimu jumla TZS 86,406,779,463 na hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya TZS 25,936,888,699 zimetumika sawa na aslimia 30.02.

d. **Mradi wa Kituo cha Mafuta na Gesi Mangapwani (CBM):** Mradi huu una lengo la kuimarisha sekta ya nishati nchini, hususan katika uhifadhi, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa jengo la ofisi, ujenzi na ufungaji wa "manifold flow meter and Scada system", ufungaji wa boya 6, dandaro 6 na miundombinu ya PLEM (Pipeline End Manifold). Kwa ujumla, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 72. Kwa mujibu wa mkataba, gharama ya ujenzi wa mradi huu ni dola za Kimarekani 17,000,000 na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya dola za Kimarekani 11,334,611.48 zimetumika.

e. **Mradi wa Bandari Kavu ya Maruhubi (ICD):** Mradi huu una lenga kuendeleza ujenzi wa Bandari Kavu (Inland Container Depot - ICD) katika eneo la Maruhubi, kwa madhumuni ya kupunguza msongamano katika bandari zetu, kurahisisha usafirishaji wa mizigo, pamoja na kuongeza ufanisi katika shughuli za uingizaji na usafirishaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi. Kwa ujumla, mradi huu umefikia asilimia 95 ya utekelezaji. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa dola za Kimarekani 4,000,000. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya dola za Kimarekani 2,850,000 zimetumika sawa na asilimia 71.25.

**Mapato na Matumizi**

65. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika la Bandari limekadiria kukusanya jumla ya **TZS 45,930,497,190.33** kupitia katika vyanzo vyake mbali mbali. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 27,991,957,276.60.** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **TZS 33,220,282,182.59** zimekusanywa sawa na **asilimia 119** kwa makadirio ya miezi tisa na **asilimia 72** ya makadirio kwa mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Shirika la Bandari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 lilipanga kutumia jumla

ya **TZS 63,520,197,971.75** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026 Shirika lilipanga kutumia jumla ya **TZS 33,322,385,061.06** ambapo **TZS 13,905,931,258** (**TZS 11,180,931,558.00** kwa matumizi ya kawaida, **TZS 2,724,999,700.00** mishahara), **TZS 16,133,050,326.32** kwa miradi ya Maendeleo na **TZS 3,283,403,476.74** kwa ajili ya malipo ya gawio na kodi za Serikali.

Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 29,631,573,226.37** zimetumika sawa na **asilimia 89** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 47** ya makadirio ya mwaka, (**TZS 2,524,999,700** ni mishahara, **TZS 8,819,502,473** kazi za kawaida, **TZS 3,541,177,825.58** kwa ajili ya malipo ya gawio na kodi za Serikali na **TZS 14,745,893,227.79** kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo.

## MALENGO YA SHIRIKA LA BANDARI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Shirika la Bandari limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuhudumia safari za Meli za kigeni 428, meli za ndani 7,653 na Majahazi 13,240. Aidha, kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika linatarajia kuhudumia tani 2,130,575 za mzigo mchanganyiko wa meli, tani 1,387,314 za mzigo wa jahazi na makontena 107,726, lita 356,052,617 za mafuta ya kuwasha (Petroleum Fuel).

ii. Kuendelea kukamilisha miradi inayoendelea ambayo ilianza utekelezaji katika kipindi cha Mwaka wa Fedha uliopita, ikiwemo Ujenzi wa Bandari ya Shumba, Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani na Fumba, kukamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi na maboresho ya bandari za Kizimkazi, Kisakasaka na Mkokotoni, kujenga maeneo ya vituo vya usafiri wa baharini (sea taxi stations) na bandari kavu.

iii. Shirika la Bandari limepanga kufanya ukarabati wa minara ikiwemo mnara wa Makunduchi, Mwana wa Mwana, ukarabati wa becon Maruhubi, ukarabati wa becon Bet-el-ras ili kuimarisha huduma za bandari.

iv. Shirika limepanga kufanya manunuzi mbali mbali ili kuimarisha huduma za bandari, manunuzi hayo yanahusu magari, mashine ya upekuzi wa mizigo na maboya ya kuongozea meli.

v. Shirika limepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi.

**MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

67. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika la Bandari Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya **TZS 38,756,000,000** na fedha iliyoko benki (cash in hand) **TZS 12,479,975,297.31** na kufanya jumla ya **TZS 51,236,388,558.16.** Pia, itatumia jumla ya **TZS 45,727,087,897.85.** Kati ya fedha hizo **TZS 8,940,579,014.00** kwa kazi za kawaida, **TZS 7,574,388,000.00** mishahara, **TZS 19,091,000,000.00** kwa kazi za maendeleo na **TZS 10,121,120,883.85** kwa malipo ya Serikali.

## E.2. SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

68. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli Zanzibar lilianzishwa rasmi chini ya Sheria nambari 3 ya mwaka 2013 (The Zanzibar Shipping Corporation Act, 2013) na limepewa jukumu la kuzisimamia na kuziendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia katika bahari ya Zanzibar.

**Utekelezaji wa kazi za Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.**

69. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi,

2026, Shirika la Meli Zanzibar limefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

a. **Ujenzi wa Boti mbili za Mwendo wa kasi:** Shirika la Meli linaendelea na Ujenzi wa Boti mbili za mwendo wa kasi zinazojengwa nchini India. Ujenzi wa boti hizo umeshafikia asilimia 50. Ujenzi boti hizo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2026.

b. **Matengenezo ya meli ya MV Mapinduzi II:** Matengenezo ya meli ya MV Mapinduzi II yamekamilika tokea Mwezi wa Novemba, 2025. Meli hiyo imeanza safari zake za Unguja na Pemba kuanzia tarehe 1 Mei, 2026.

c. **Utoaji wa Huduma za Kusafirisha nishati ya mafuta kwa kutumia Meli ya MT Ukombozi II:** MT Ukombozi II inaendelea na safari zake za kuchukua nishati ya mafuta kutoka Tanzania Bara na kuyaleta Zanzibar. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 meli hii ilipangiwa safari 30 na hadi kufikia Machi, 2026 imefanya safari 33 sawa na asilimia 110 ya makadirio. Jumla ya TZS 4,290,000,000 zimepatikana kwa safari hizo.

d. **Utoaji wa Huduma za Uwakala wa Meli:** Shirika linaendelea kutoa huduma za uwakala wa Meli. Kwa Mwaka 2025/2026 Shirika lilipanga kuhudumia meli 157 na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya meli 145 zilihudumiwa sawa na asilimia 92 ya meli zilizokadiriwa kwa mwaka. Aidha, Shirika lilipanga kuhudumia makontena 27,008 kwa kipindi hicho, hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya makontena 26,652 yamehudumiwa sawa na asilimia 99 ya makadirio.

e. **Matengenezo ya Majengo ya Afisi:** Shirika la Meli Zanzibar limefanikiwa kufanya matengenezo ya majengo ya Afisi kuu Unguja na Dar es salaam. Jumla ya TZS 296,126,725 zilitumika kwa Afisi kuu na jumla ya TZS 88,439,820 kwa Afisi ya Dar es salaam.

f. **Kuwajengea uwezo wafanyakazi:** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Shirika la Meli lilipanga kuwajengea uwezo wafanyakazi 35 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya wafanyakazi 22 walipatiwa mafunzo katika fani tofauti sawa na asilimia 62.8 ya makadirio ya mwaka.

**Mapato na Matumizi**

**70.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika la Meli lilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 14,373,657,800** kutoka katika vyanzo vyake. Hadi kufikia Machi, 2026, Shirika limekusanya jumla ya **TZS 12,236,013,286** sawa na **asilimia 85** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya **TZS 13,711,591,200** kwa kazi za kawaida na Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 8,767,433,285** zimetumika sawa na **asilimia 63.9** ya makadirio ya mwaka.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MELI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**71.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika la Meli limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kusafirisha abiria na mizigo kwa kutumia Meli ya MV Mapinduzi II. Jumla ya abiria 54,400 wanatarajiwa kusafirishwa na tani 16,400 za mizigo zinatarajiwa kuchukuliwa baina ya Visiwa vya Unguja na Pemba.

ii. Kuendelea na Ujenzi wa boti mbili za mwendo wa kasi ambazo zitafanya kazi ya usafirishaji abiria baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es salaam ambazo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2026.

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 30 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa tija na ufanisi.

iv. Kuendelea kutoa huduma za uwakala kwa meli zote zinazokuja katika bahari ya Zanzibar ambapo Shirika limepanga kuhudumia meli 222 za Makontena, ship to ship (STS), kichele, mafuta, kijeshi na meli za kitalii.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Shirika limekadiria kukusanya jumla ya **TZS 32,515,988,327** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa upande wa matumizi, Shirika limepanga kutumia **TZS 27,296,165,429** kwa kazi za kawaida na **TZS 5,065,901,371** kwa kazi za Maendeleo.

## E.3. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka Usafiri Baharini, kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Baharini Nambari 5 ya Mwaka 2006 na Sheria ya Mamlaka ya Usafiri Baharini nambari 3 ya Mwaka 2009, ina jukumu la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza sekta ya usafiri wa baharini, ikiwemo usajili na ukaguzi wa meli, kuhakikisha usalama na ulinzi wa meli na bandari, kudhibiti uchafuzi wa mazingira ya bahari, kutoa leseni na vyeti kwa mabaharia na vyombo vya baharini, kuchunguza ajali za baharini, kusimamia maslahi na ustawi wa mabaharia, pamoja na kuratibu shughuli za utafutaji na uokozi baharini.

**Utekelezaji wa Kazi za Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.**

**74.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

a. **Usajili wa Meli za Kimataifa na Meli za ndani:** Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 Mamlaka ilikadiria kusajili jumla ya Meli 256, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2026 jumla ya Meli 112 zilisajiliwa sawa na asilimia 44 ya makadirio. Kati ya Meli hizo 96 za Kimataifa na Meli 16 za ndani zilisajiliwa. Upungufu huo unatokana na Mamlaka kusitisha kwa muda usajili wa meli za Kimataifa kwa ajili ya kumuezesha Naibu Msajili, Kufanya uhakiki wa meli zilizopo. Aidha, Mamlaka imeingia mkataba na Kampuni ya International Maritime Expert (IME) ya Dubai kwa ajili ya kuhakikisha usajili wa Meli za Kimataifa unafikia malengo na unatekelezwa kwa ufanisi na kuzingatia matakwa ya Kimataifa.

b. **Usajili wa Vyombo Vidogo Vidogo na Leseni za Mabaharia:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Mamlaka ilipanga kusajili jumla ya vyombo vidogo vidogo 1,500 hadi kufikia Machi 2026, Mamlaka ilisajili vyombo vidogo vidogo 1,157 sawa na asilimia 77 ya makadirio.

c. **Kuthibitisha Vyeti vya Mabaharia wa Kigeni:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipanga kuthibitisha vyeti 600 vya Mabaharia vya ngazi ya maofisa wanaofanya kazi katika meli za Kimataifa (TZIRS). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya Mabaharia 1,314 wamethibitishwa vyeti vyao vya umahiri sawa na asilimia 219 ya makadirio.

d. **Utoaji wa Vitabu vya Mabaharia (Discharge Book):** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipanga kutoa vitabu vya Mabaharia 1800, hadi kufikia Machi 2026, jumla ya Mabaharia 1,219 wamepewa vitabu sawa na asilimia 68 ya makadirio.

e. **Kuthibitisha Vyeti na Mikataba ya Mabaharia wanao safiri Nje ya Nchi:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipanga kuthibitisha vyeti 192 hadi

kufikia Machi 2026, Mamlaka imeweza kuthibitisha vyeti 186 sawa na asilimia 97 ya makadirio. Aidha, Mamlaka ilipanga kuthibitisha Mikataba 960 ya Mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia Kampuni ya DANAOS hadi kufikia Machi 2026, Mamlaka ilithibitisha Mikataba 916 sawa na asilimia 95 ya makadirio.

f. **Kutoa Vitambulisho vya Mabaharia (Seafares ID):** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipanga kutoa vitambulisho 600 ambapo hadi kufikia Machi 2026, Mamlaka imeweza kutoa vitambulisho 305 sawa na asilimia 51 ya makadirio.

g. **Ukaguzi wa Meli:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipanga kukagua jumla ya Meli 95 za ndani, hadi kufikia Machi 2026, jumla ya Meli 67 zenye GT 110,052 sawa na asilimia 71 ya makadirio. Kati ya Meli hizo 30 zenye GT 40,256 zilifanyiwa ukaguzi wa mwaka wa kiusalama, na Meli 19 zenye GT 38,157 zilifanyiwa ukaguzi wa kushtukiza, Meli 12 zenye GT 28,044 zilifanyiwa ukaguzi wa awali na Meli 1 yenye GT 490, ilifanyiwa ukaguzi wa dharura na Meli 5 zenye GT 3,105 zilifanyiwa ukaguzi wa chelezoni.

h. **Ukusanyaji wa Takwimu za Abiria:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilikadiria kusimamia jumla ya abiria 1,800,000 katika Bandari za Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2026, idadi ya abiria waliosafiri ni 1,510,671 sawa na asilimia 84 ya makadirio. Kati ya abiria hao, waliosimamiwa kati ya Unguja/Pemba ni 263,970 Pemba /Unguja 285,707 Zanzibar/Dar 923,594 na Pemba/Tanga ni 37,400.

i. **Utoaji leseni kwa Kampuni na Taasisi mbali mbali zinazotoa huduma za Usafiri Baharini:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilikadiria kutoa leseni 377 kwa Taasisi zinazotoa huduma za Usafiri Baharini, hadi kufikia Machi 2026, Mamlaka imefanikiwa

kutoa Leseni 142, sawa na asilimia 38 ya makadirio. Huduma zilizotolewa ni pamoja na watoaji mizigo Bandarini (clearing and forwarding), Diving Center, Water Sport, Kampuni yenye Meli moja na Kampuni zenye Meli zaidi ya moja na Wakala wa kuuza ticket.

j. **Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Mamlaka:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipanga kuwajengea uwezo wafanyakazi 39 na hadi kufikia Machi 2026 Mamlaka imefanikiwa kuwajengea uwezo wafanyakazi 23 katika fani mbali mbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kati ya hao wafanyakazi 9 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu, wafanyakazi 6 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi.

k. **Kutayarisha Miongozo na Kanuni za Mamlaka:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka imetayarisha Rasimu 3 za Kanuni, ambazo ni Kanuni ya Sea Tax Regulation ya Mwaka 2025, Kanuni ya kazi za Mabaharia (Maritime Labour Regulations) ya Mwaka 2025 na Kanuni ya Usajili wa Mabaharia ya Mwaka 2026. Aidha, Mamlaka ilipitia Kanuni (2) ambazo ni Kanuni ya Usajili wa Vyombo vya Baharini na utoaji leseni ya Mwaka 2007 na Kanuni ya Usalama wa Vyombo Vidogo Vidogo ya Mwaka 2008.

l. **Kukamilisha mfumo wa utoaji vibali kwa Mabaharia:** Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kukamilisha mfumo wa utoaji vibali kwa Mabaharia Electronic Seafarers Identity Document System (e-SID) ambapo huduma itaweza kutolewa na Mamlaka badala ya kutolewa na Ofisi ya ZAN ID ambayo hupelekea kutumia muda zaidi katika upatikanaji wake.

m. **Kuanza hatua za awali za mfumo wa Usajili Mabaharia Zanzibar Seafarer's Digital Registry (ZSDR) wanaokwenda kufanya kazi katika Meli za Kimataifa:** Mfumo huo utakuwa na faida ya kurahisisha uthibitishwaji wa

vyeti vya Mabaharia vinavyotolewa na Kampuni ya DANAOS, na kuiwezesha Mamlaka kuwa na taarifa kamili za Mabaharia wanaokwenda kufanya kazi katika Meli ikiwemo kujua aina ya meli, na kada anayoifanyia kazi.

**Mapato na Matumizi**

**75.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 8,797,036,295** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Mamlaka ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 6,612,777,222** na hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS 5,868,704,253** zimekusanywa sawa na **asilimia 89** ya makadirio ya robo tatu na **asilimia 66.7** kwa makadirio ya mwaka. Upungufu wa mapato unatokana na Mamlaka kusitisha kwa muda Usajili wa meli mpya ili kuhakiki meli zilizopo.

Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, ilikadiria kutumia jumla ya **TZS 8,463,979,092** kwa kazi za kawaida, Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, ilipanga kutumia **TZS 6,365,800,569** na hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS 2,645,754,560** zimetumika sawa na **asilimia 42** ya makadirio ya robo tatu na **asilimia 31** kwa makadirio ya bajeti ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **TZS 1,451,558,186** ni mishahara na **TZS 1,194,196,374** kwa kazi za kawaida.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.**

**76.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendelea kuimarisha Usajili wa Meli za Kimataifa kwa kushirikiana na Kampuni ya International Maritime Expert ya Dubai.

ii. Kusajili Meli 20 za ndani, kutoa Leseni 1,800 kwa Vyombo Vidogo Vidogo, Vitabu 1,440 vya Mabaharia (Discharge Books), kuthibitisha Mikataba 960 ya Mabaharia, kuthibitisha Vyeti 240 vya mafunzo ya Ulinzi Melini (Maritime Security Awareness) kwa Mabaharia wanaosafiri na Meli za Nje kupitia Kampuni ya DANAOS, kutoa vitambulisho vya Mabaharia Seafares ID 420, kuthibitisha Vyeti 600 vya Mabaharia wa Kigeni (Endorsements), kutoa Leseni 377 zinazohusu huduma za Usafiri wa Bahari pamoja na kufanya ukaguzi wa Meli 120 za ndani.

iii. Kuwajengea uwezo Wafanyakazi 37 wa Mamlaka kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na kuimarisha mazingira ya kutendea kazi.

iv. Kufanya Mikutano 20 na Wadau wa Sekta ya Usafiri Baharini na Kuwaelimisha Wananchi kwa kufanya vipindi vya TV na Redio juu ya utunzaji wa mazingira ya Bahari na usalama wa usafiri baharini.

v. Kusimamia utatuzi wa changamoto za Mabaharia pamoja na maslahi yao.

vi. Kuendelea na marekebisho ya hoja za ukaguzi wa IMSAS [International Members State Audit Scheme] kwa mujibu wa mpango wa marekebisho ulioandaliwa.

vii. Kuwapatia vifaa vya uokozi watumiaji wa Vyombo vya usafiri wa vyombo vidogo vidogo ambao hawana uwezo wa kumiliki vifaa hivyo.

viii. Kutoa elimu kwa Mabaharia na Manahodha juu ya usalama na udhibiti wa ajali za Baharini kwa watumiaji wa Vyombo Vidogo Vidogo.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**77.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mamlaka ya Usafiri Baharini imekadiria kukusanya jumla

ya **TZS 6,334,937,928** na imepanga kutumia jumla ya **TZS 6,334,262,960** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, jumla ya **TZS 2,237,956,200** ni mishahara na **TZS 4,096,306,760** kwa kazi za kawaida.

## E.4. MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilianzishwa kwa Sheria ya Usafiri Barabarani Zanzibar, Nam. 7 ya 2003 katika marekebisho ya 10 ya mwaka 2019 ambayo imepewa jukumu la kusimamia watumiaji wa usafiri barabarani, utoaji wa huduma za usafiri barabarani pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani.

**Utekelezaji wa Malengo ya Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.**

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imetekeleza kazi zifuatazo: -

a. **Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:** Jumla ya vyombo vya moto 76,629 vilipangwa kukaguliwa na hadi kufika Machi, 2026 jumla ya vyombo vya moto 58,217 vimekaguliwa sawa na asilimia 76 ya makadirio ya mwaka. Kati ya vyombo hivyo 50,237 vimekaguliwa Unguja na 7,980 vimekaguliwa Pemba.

b. **Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji:** Jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 24,405 zilipangwa kutolewa na hadi kufikia Machi, 2026 ruhusa za njia na usafirishaji 22,089 kwa gari mbalimbali zinazotoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo zimetolewa sawa na asilimia 90.5 ya makadirio ya mwaka. Kati ya ruhusa hizo, 19,315 zimetolewa Unguja na ruhusa 2,774 zimetolewa Pemba.

c. **Utoaji wa Leseni kwa Gari za Biashara:** Jumla ya leseni

kwa gari za biashara 23,198 zilipangwa kutolewa na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya leseni 18,517 za usafirishaji zimetolewa kwa gari za biashara aina mbalimbali zinazotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo sawa na asilimia 80 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, leseni 16,406 zimetolewa Unguja na leseni 2,111 zimetolewa Pemba.

d. **Utoaji wa Vyeti vya Umahiri kwa Madereva (Certificate of Competence):** Mamlaka ilipanga kutoa vyeti vya umahiri kwa madereva 19,305 na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya vyeti vya umahiri 13,175 vimetolewa kwa madereva sawa na asilimia 68 ya makadirio ya mwaka. Ikiwa vyeti vya udereva 10,016 vimetolewa Unguja na 3,159 vimetolewa Pemba.

e. **Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva:** Jumla ya beji 11,949 za utingo na madereva wa vyombo vya biashara aina mbalimbali zilipangwa kutolewa na hadi kufikia Machi 2026, jumla ya beji 7,743 zimetolewa sawa na asilimia 65 ya makadirio ya mwaka. Kati ya beji hizo 7,169 zimetolewa Unguja na 574 zimetolewa Pemba.

f. **Utoaji wa Leseni za Madereva Wanafunzi (Learner Licences):** Jumla ya leseni za madereva wanafunzi 28,860 zilipangwa kutolewa na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya leseni 15,004 za madereva wanafunzi zimetolewa sawa na asilimia 52 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, 13,613 zimetolewa Unguja na 1,391 zimetolewa Pemba.

g. **Utoaji wa Vibali kwa madereva Wageni:** Jumla ya vibali kwa madereva wageni 35,400 vilipangwa kutolewa hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya vibali 25,629 vya ruhusa ya kuendesha vyombo vya moto kwa wageni vimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 72 ya makadirio ya mwaka. Kati ya vibali hivyo 25,493 vimetolewa Unguja na 136 vimetolewa Pemba.

h. **Utoaji wa Mafunzo kwa Madereva na Utingo:** Mamlaka ilipanga kuwapatia mafunzo madereva na utingo 6,300 na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya madareva na utingo 3,858 wamepatiwa mafunzo ya usalama barabarani sawa na asilimia 61.2 ya makadirio. Kati ya hao madereva 3,619 wamepatiwa Unguja na 239 wamepatiwa mafunzo Pemba.

i. **Mradi wa ZIMS - Zartsa Integrated Management System:** Mamlaka imeendelea na matumizi ya mfumo wa ZIMS kwa kufanya mabadiliko ya utoaji wa huduma zake za kila siku kutoka kutumia utaratibu wa zamani na kuhamia katika matumizi ya mifumo ambapo huduma zote zinapatikana kwa njia ya mtandao kupitia mifumo hiyo. Huduma zenyewe ni: Utoaji wa vibali (Permit); Utoaji wa Leseni za kuendeshea vyombo vya moto; Utoaji wa beji; Utoaji wa vibali kwa madereva wanaoendesha vyombo vya moto vya Serikali pamoja na Upasishaji wa vyombo vya moto.

**Mapato na Matumizi**

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 6,177,981,800** na kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2026 ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 4,636,382,350** kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato kwa Unguja na Pemba na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 4,817,647,790** zimekusanywa sawa na **asilimia 104** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 77.9** kwa makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa Matumizi, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilipanga kutumia jumla ya **TZS 6,177,981,800** ikiwa **TZS 2,073,974,864** ni mishahara, **TZS 2,104,186,936** kazi za kawaida na **TZS 2,000,000,000** ni mchango wa Mamlaka kwa Serikali kuu. Aidha, kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2026 Mamlaka ilipanga kutumia jumla ya **TZS 4,640,242,350**

ikiwa **TZS 1,555,346,148** ni mishahara, **TZS 1,584,896,202** kazi za kawaida na **TZS 1,500,000,000** ni mchango wa Mamlaka kwa Serikali kuu.

**81.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS 4,526,929,406** zimetumika kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo sawa na **asilimia 98** ya makadirio. Kati ya fedha hizo, **TZS 1,507,789,951** ni mishahara, **TZS 829,350,259** ni matumizi ya kawaida, **TZS 1,500,000,000** zimewasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na **TZS 689,789,200** zimewasilishwa kwa Mwekezaji wa Kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.**

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kusimamia utoaji wa huduma za usafiri na usalama barabarani kwa kutoa leseni za madereva wanafunzi 26,000, kuvifanyia ukaguzi vyombo vya moto 82,223, majaribio ya udereva kwa madereva 23,500, kutoa vibali 29,000 kwa madereva wageni, leseni kwa vyombo vya Biashara 25,200, kutoa ruhusa za njia za usafirishaji 43,000, beji za madereva na utingo 17,000, kutoa vibali kwa madereva wa Serikali vipatavyo 3,000, kusajili vyombo vya moto 15,244 pamoja na kutoa leseni za udereva 37,728.

ii. Kuandaa semina, warsha, makongamano kwa lengo la kutoa uelewa kwa wadau wa Sekta ya Usafiri Barabarani.

iii. Kuwapatia mafunzo madereva na utingo wa vyombo vya moto vya Serikali na Binafsi wapatao 6,300.

iv. Kuandaa tathmini ya ajali kuhusiana na usafiri na

usalama barabarani pamoja na kuandaa mtaala mpya ya programu za udereva.

v. Kuendelea kuweka kamera za usalama barabarani ili kubaini na kudhibiti madereva wote wanaotenda makosa ya barabarani.

vi. Kujenga kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto cha kisasa Pemba pamoja na vituo viwili vya utahini wa madereva Unguja na Pemba.

vii. Kufanya uhakiki wa leseni za udereva na kutoa leseni mpya.

viii. Kufanya mapitio ya Sheria ya Usalama Barabarani no. 7 ya 2003.

ix. Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi kuu za Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imekadiria kukusanya jumla ya **TZS 6,000,000,000** kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ya ndani na imepanga kutumia jumla ya **TZS 6,000,000,000.** Kati ya fedha hizo, **TZS 2,278,279,850** ni kazi za kawaida, **TZS 1,471,720,150** ni mishahara, **TZS 2,250,000,000** ni mchango kwa Serikali Kuu.

## E.5. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

**84.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria namba 8 ya Mwaka 2011 na ina jukumu la kuviendesha, kuvisimamia na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali pamoja na kusimamia usalama wa safari za abiria, ndege na mizigo katika viwanja vya ndege vya Serikali. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wakati wa utekelezaji wa majukumu yake inazingatia taratibu na

sheria zote za uendeshaji wa viwanja kama zinavyoelekezwa na Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA) na International Civil Aviation Organization (ICAO).

**Utekelezaji wa Kazi za Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**85.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

a. **Kuhudumia Safari za Ndege, Abiria na Mizigo:** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea kutekeleza kazi zake za kawaida za kuhudumia safari za ndege, abiria na mizigo katika viwanja vya Ndege Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya safari za ndege 58,176 zimehudumiwa sawa na asilimia 83 ya makadirio ya safari 70,294 zilizopangwa kuhudumiwa kwa mwaka. Kati ya safari hizo, safari za ndege 53,762 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na safari za ndege 4,414 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Safari za ndege za Kimataifa zilikuwa ni 11,853 na safari za ndani zilikuwa ni 41,909. **Kiambatanisho namba 7A** kinahusika.

   Aidha, jumla ya abiria 2,108,239 wamehudumiwa sawa asilimia 90.8 ya makadirio ya abiria 2,321,400 waliopangwa kuhudumiwa kwa mwaka. Kati ya hao, abiria, 2,021,797 walihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na abiria 86,442 walihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Abiria 1,237,102 ni wa safari za kimataifa na abiria 871,137 ni wa safari za ndani. Jumla ya Abiria waliopita (transit passengers) ni 202,882 ikiwa abiria 202,877 walipita katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa

wa Abedi Amani Karume na abiria 5 walipita katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. **Kiambatanisho namba 7B** kinahusika.

Kwa upande wa mizigo, jumla ya tani 4,111 zilihudumiwa katika uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume sawa na asilimia 116 ya tani 3,543 zilizokadiriwa kwa mwaka.

Kwa upande wa huduma za Ndege, Mamlaka imehudumia jumla ya Mashirika na Kampuni za ndege 81 za ndani na nje katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar katika kipindi cha miezi tisa. **Kiambatanisho namba 7C** kinahusika.

b. **Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeimarisha ulinzi na usalama kwa kufanya ukarabati wa mashine za X-ray na vifaa vya TEHAMA, kuboresha mifumo ya CCTV, kufanya tathmini za hatari katika maeneo muhimu ya uwanja, pamoja na kutoa mafunzo ya ulinzi na usalama kwa wafanyakazi 121 ili kuongeza ufanisi wa huduma.

c. **Ukarabati wa Jengo la Abiria la Terminal 1:** Serikali imeamua kulifanyia usanifu na maboresho makubwa jengo hilo pamoja na kulifanyia utanuzi ili liendane na hadhi za kimataifa. Usanifu, Ukarabati na Ujenzi wa Jengo la abiria TB1 umeanza rasmi tarehe 18/05/2024. Mkandarasi wa jengo hili ni Kampuni ya Estim Enterprises Company Limited. Jengo hilo litakuwa na kumbi mbili ambazo zitahudumia wageni kutokana na hadhi na madaraja yao. Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 16,541,884,800 hadi kukamilika kwake na hadi kufikia Machi, jumla ya TZS 15,817,707,580.83 zimetumika. Kwa ujumla ukarabati na ujenzi wa jengo la TB1 umekamilika kwa asilimia 100.

d. **Kuendeleza Ujenzi wa Kituo cha Biashara (Business Center) katika Jengo la Terminal 3:** Mamlaka imefanikiwa kuimarisha mazingira ya biashara katika Uwanja wa AAKIA kwa kuingia mkataba na Kampuni ya Estim Enterprise kwa ajili ya kujenga na kuendesha Kituo cha Biashara (Business Center) katika Uwanja wa AAKIA. Aidha, ujenzi huu utajumuisha maofisi, huduma za mabenki, maduka na mikahawa, Ujenzi huu umeanza rasmi tarehe 17/4/2024. Hadi kufikia Machi, 2026 mradi huu umefikia asilimia 90% ya utekelezaji wake.

**Mapato na Matumizi**

86. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 55,395,962,119** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 43,327,544,959.94** kupitia vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Machi, 2026, jumla ya **TZS 42,253,453.878.22** zimekusanywa sawa na **asilimia 97** ya makadirio ya robo tatu na **asilimia 79** ya makadirio ya mwaka.

87. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipanga kutumia jumla ya **TZS 55,395,962,119** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiria kutumia jumla ya **TZS 43,273,714,652**. Kati ya fedha hizo,**TZS 19,443,080,197** ni kwa matumizi mengineyo, **TZS 10,678,500,000** ni mishahara na **TZS 13,152,134,455** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2026, jumla ya **TZS 40,281,097,503.36** zimetumika sawa na **asilimia 93** ya makadirio ya robo tatu na **asilimia 73** ya makadirio ya mwaka, Kati ya fedha hizo **TZS 11,062,376,737.14** ni mishahara, **TZS 16,724,413,321.19** ni matumizi mengineyo na **TZS 12,494,307,445.03** ni kwa kazi za maendeleo.

**MALENGO YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.**

**88.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kufanya zoezi kamili la uokoaji wa ajali ya ndege, ununuzi wa gari ya zimamoto na kuvifanyia matengenezo vifaa vya ulinzi na usalama.

ii. Mamlaka imepanga kuimarisha miundombinu kwa kuendelea na Awamu ya Pili ya Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria la (TB 2) katika uwanja wa AAKIA, ujenzi wa maegesho ya ndege (apron), ujenzi wa Jengo Jipya la Kuongozea Ndege (Control Tower), kuanza ujenzi wa jengo la ofisi za Mamlaka kwa hatua za awali, kuweka taa za kuongozea ndege (AGL) katika uwanja wa AAKIA, ujenzi wa karakana ya matengenezo ya ndege, kuendeleza ujenzi wa uwanja wa ndege Nungwi, Ujenzi wa daraja la kuunganisha TB2 na TB3 pamoja na ujenzi wa kituo Kipya cha Biashara.

iii. Kuimarisha miundombinu ya biashara kwa kukamilisha ujenzi wa Kituo kipya cha Biashara (Bussiness Centre) katika jengo la abiria la TB 3.

iv. Mamlaka imepanga kuhudumia abiria 2,507,112, Ndege 71,700 na Mzigo tani 4,439 katika viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**89.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekadiria kukusanya jumla ya **TZS 57,258,093,000** na imepanga kutumia jumla ya **TZS 57,258,093,000.** Kati ya fedha hizo, **TZS**

**3,059,923,728** zitatumika kwa mishahara, **TZS 5,510,380,852** kwa kazi za kawaida, **TZS 7,749,028,420** kwa kazi za maendeleo na **TZS 40,938,760,000** kwa ajili ya uendeshaji wa AAKIA.

## E.6. BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

90. **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo inasimamia shughuli zinazofanywa na Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo. Majukumu makubwa ya Bodi ni kusajili Wasanifu, Wahandisi, Wakadiriaji Majengo, Makampuni ya kiushauri ya kada hizo, kufuatilia mwenendo wa kazi wanazozifanya pamoja na kuwaendeleza Wataalamu wa kada hizo kwa kuratibu mikutano na semina zinazohusiana na kazi za wataalamu hao.

**Utekelezaji wa Malengo ya Bodi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.**

91. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

a. **Kusajili Wataalamu wa Ujenzi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Bodi ilikadiria kusajili jumla ya wataalamu 180 na kampuni za ushauri 20 na hadi kufikia Machi 2026, imefanikiwa kusajili jumla ya wataalamu 122 sawa na asilimia 67.7 ya makadirio na kampuni za ushauri 14 sawa na asilimia 70 ya makadirio.

b. **Usajili wa miradi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Bodi ilikadiria kusajili miradi 400 na hadi kufikia Machi 2026, Bodi imefanikiwa kusajili miradi 345 sawa na asilimia 86 ya makadirio ya miradi mbali mbali ya ujenzi.

c. **Kufanya ukaguzi katika maeneo ya Ujenzi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi imekadiria kukagua miradi 300 na hadi kufikia Machi 2026, Bodi imefanikiwa kukagua miradi 186 sawa na asilimia 62 ya makidirio ya mwaka.

d. **Mfumo wa Usajili wa Kidigitali:** Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Bodi imefanikiwa kuanza matumizi ya mfumo wa usajili wa wataalamu na miradi ili kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma za Bodi kwa ufanisi zaidi.

e. **Kuwaendeleza wahitimu:** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Bodi imefanikiwa kuwajengea uwezo wahitimu (Graduates) 26 kupitia programu ya mafuzo ya vitendo (Structural Apprenticeship Program for Architects, Engineers and Quantity Surveyors - SAPAEQ) ambapo wahitimu 20 wa kike wananufaika katika Programu ya SEAP kupitia mashirikiano na Bodi ya Wahandisi Tanzania (ERB) na wahitimu 6 wananufaika katika Programu ya SAPAEQ inayosimamiwa na kudhaminiwa na Bodi.

f. **Kutoa elimu kwa watendaji wa Bodi na Wadau:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ilipanga kutoa elimu ya kujengea uwezo kwa kusomesha watendaji 10 na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya watendaji 6 wamepatiwa mafunzo sawa na asilimia 60 ya makadirio.

g. **Kukuza mashirikiano na Taasisi za nje ya Zanzibar:** Bodi imeendelea kushirikiana kwa karibu na Bodi za Tanzania (ERB na AQRB) katika kutekeleza maeneo mbali mbali ya ushirikiano na katika muendelezo huo, Bodi imeshiriki mikutano mitano ya kubadilishana uzoefu, mikutano mitatu imefanyika Tanzania Bara na miwili Zanzibar.

h. **Programu ya Kuwaendeleza Wataalamu:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Bodi ilipanga kufanya mafunzo

mara (2) kwa wataalamu wa ujenzi na hadi kufikia Machi, 2026 Bodi imefanikiwa kufanya mafunzo mara moja yanayohusu Usuluhisho wa migogoro katika miradi ya ujenzi. Jumla ya wataalamu 150 walishiriki katika mafunzo hayo.

**Mapato na Matumizi**

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilikadiria kukusanya Jumla ya **TZS 833,574,000** kwa mwaka na kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2026, ilikadiria kukusanya Jumla ya **TZS 630,944,000** na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 757,227,538** zimekusanywa sawa na **asilimia 120** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 90.84** ya makadirio ya mwaka. **Asilimia 50** ya makusanyo yameingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa ni mchango wa Bodi.

Kwa upande wa matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ilipanga kutumia jumla ya **TZS 678,586,500.** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2026, Bodi ilipanga kutumia jumla ya **TZS 479,651,500** na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 371,530,141** zimetumika sawa na **asilimia 77.6** ya makadirio ya bajeti kwa kipindi cha miezi tisa na **asilimia 55** ya makadirio ya bajeti kwa mwaka.

**MALENGO YA BODI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.**

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027, Bodi ya Usajii Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuendeleza na Kuimarisha matumizi ya mifumo katika kazi za Usajili wataalamu (online registration) ambapo imepanga kusajili wataalamu 170 wa ujenzi na kusajili miradi ya Ujenzi 450.

ii. Kuendelea kuwasimamia wahitimu 30 katika mafunzo ya vitendo ya fani za Usanifu, Uhandisi na Ukadiriaji

Majengo katika programu inayofadhiliwa na Bodi. Aidha, Bodi itaendelea kushajihisha wahitimu kujiunga na program ya mafunzo ya vitendo kwa kushirikiana na Makampuni ya Kishauri na Wakandarasi nchini pamoja na Washirika wa Maendeleo.

iii. Kuendelea na programu za kuwaendeleza Wataalamu wenye kada za Usanifu, Uhandisi na Ukadiriaji Majengo na wengineo (Professional Development) kwa kutayarisha mafunzo mara mbili ya kuwaendeleza wataalamu pamoja na kufanya Kongamano la Mwaka.

iv. Kuifainyia marekebisho Sheria Nam 5 ya mwaka 2008 ya Uwanzishwaji wa Bodi ili kuongeza wigo wa kada kwenye maeneo yote ya kazi na kuainisha mambo muhimu yanayoendana na wakati wa sasa.

v. Kuendelea kuimarisha uhusiano kwa kutelekeza mpango kazi na Taasisi zilizoingia mkataba wa mashirikiano (MoU) na Bodi ambazo ni IAESZ ya Zanzibar na AQRB, ERB za Tanzania pamoja na kuanzisha mashirikiano ya Taasisi zilizopo katika EAC na SADC.

vi. Kuwajengea uwezo watendaji 12 wa Bodi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**94.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027, Bodi ya Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imekadiria kukusanya jumla ya **TZS 1,350,000,000** na kutumia jumla ya **TZS 675,000,000** kwa kazi za kawaida. **Asilimia 50** ya makusanyo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

## E.7. BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI.

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ina jukumu la kusajili Wakandarasi na kutunza Daftari la Wakandarasi, kusimamia shughuli za Wakandarasi, kupanga

na kutoa mafunzo, warsha, makongamano juu ya masuala yanayohusiana na ujenzi, kuweka vigezo na madaraja mbalimbali ya Wakandarasi kwa ajili ya usajili pamoja na kupokea, kuchunguza na kusikiliza malalamiko dhidi ya Wakandarasi.

**96.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. **Usajili wa Wakandarasi Wapya:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kusajili Wakandarasi wapya 72 na hadi kufikia Machi, 2026 imefanikiwa kusajili Wakandarasi wapya 131 Unguja na Pemba, sawa na asilimia 182 ya makario ya mwaka.

b. **Usajili wa Miradi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ilipanga kusajili miradi 400 na hadi kufikia Machi, 2026 imefanikiwa kusajili miradi 218 sawa na asilimia 54.5 ya makadirio ya mwaka.

c. **Ukaguzi wa Miradi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ilipanga kukagua miradi 380 na hadi kufikia Machi, 2026 imefanikiwa kufanya ukaguzi wa miradi 347 Unguja na Pemba sawa na asilimia 91 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Bodi imechukuwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa Wakandarasi 148 waliokiuka sheria.

**Mapato na Matumizi**

**97.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 1,771,346,000** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 1,415,791,400.** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 941,104,500** zimekusanywa sawa na **asilimia 66.4** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 53.3** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kutumia jumla ya **TZS 885,673,000** na kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia **TZS 770,973,000** na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 440,103,699.8** zimetumika sawa na **asilimia 57.08** ya makadirio ya miezi tisa na **asilimia 50** ya makadirio ya bajeti.

**MALENGO YA BODI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.**

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027, Bodi ya Usajii wa Wakandarasi imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendelea na usajili wa Wakandarasi wapya 150 na kuwapandisha madaraja Wakandarasi ambao walishasajiliwa na Bodi.

ii. Kuendelea na usajili wa miradi 410 ambayo inatekelezwa na wakandarasi hapa Zanzibar.

iii. Kufanya ukaguzi wa miradi 430 ili kuhakikisha ujenzi wote unaofanyika nchini unatekelezwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za Bodi ya Usajili wa Wakandarasi.

iv. Kuandaa Semina, Mikutano na Mafunzo mbali mbali kwa Wakandarasi, wadau wa sekta ya ujenzi, Wajumbe na Watendaji wa Bodi ili kuwajengea uwezo katika majukumu yao ya kila siku.

v. Kushajihisha wanafunzi kupenda masomo ya Sayansi kwa lengo la kupata wataalamu wa fani mbali mbali katika sekta ya ujenzi.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

**99.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imekadiria kukusanya Jumla ya **TZS 1,919,001,200** kupitia vyanzo vyake vya mapato. **Asilimia 50** ya makusanyo hayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa upande wa matumizi, Bodi imepanga kutumia jumla ya **TZS 959,500,599.5** kwa kazi za kawaida.

## F. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO

100. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Uchukuzi. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (TCAA) na Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (TMA).

101. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zinashabihiana kimajukumu na kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi hapa Zanzibar. Wizara hizo ni: - Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi. Mashirikiano ya Wizara hizi pamoja na Taasisi zake zimechangia sana kukuza Sekta za Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi hapa Zanzibar. Napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza Wizara hizo na Taasisi zake kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara yetu.

## G. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA UJENZI NA UCHUKUZI.

102. **Mheshimiwa Spika,** Sekta binafsi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi Zanzibar. Serikali inatambua na kuthamini mchango huo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi kupitia utoaji wa huduma bora zinazochochea maendeleo ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, kuongeza Pato la Taifa, pamoja na kutoa ajira kwa wananchi wengi. Wizara itaendelea kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na kuweka mazingira bora ya kisera na kiuwekezaji yatakayowezesha sekta hizo kuendelea kutoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo na ustawi wa uchumi wa Zanzibar.

**103. Mheshimiwa Spika,** Nakuchukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi binafsi zinazotoa huduma mbalimbali za ujenzi na Uchukuzi kwa kazi nzuri wanayoifanya na naziomba ziendelee kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi. Aidha, nizipongeze Kampuni ya DNATA, Kampuni ya SEGAP, Kampuni ya Emirate leisure. Kampuni ya ZMT, Fumba Port, Kampuni ya ZF DEVCO, Kampuni ya ZENJI Machandise na Kampuni ya Ndani Investment Cooparation kwa ushirikiano na mchango wao mkubwa wanaoutoa kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na kuhakikisha kuwa huduma za Usafiri wa Anga, huduma za bandari pamoja na huduma za usafiri wa barabara zikuwa bora na zenye ufanisi hapa Zanzibar.

## H. MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

**104. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kuwasilisha utekelezaji wa programu mbali mbali zinazosimamiwa na Wizara pamoja na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, kwa ruhusa yako sasa, naomba kuwasilisha muelekeo wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama ifuatavyo:-

### H.1. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**105. Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo na miongozo mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, Sera ya Taifa ya Usafiri Zanzibar (2008), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan - 2007) pamoja na Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar - ZADEP (2026 - 2030). Aidha, bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia Sera mbalimbali za sekta mtambuka za Taifa, Ilani ya Uchaguzi

ya Chama cha Mapinduzi (2025 - 2030), Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan), Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika ufunguzi wa Baraza la 11 la Wawakilishi pamoja na ahadi na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Vilevile, maandalizi ya mashindano ya Mpira wa Miguu wa Mataifa ya Afrika (AfCON) yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027, ambapo Tanzania ni miongoni mwa nchi mwenyeji wa mashindano hayo, yamepewa kipaumbele katika maandalizi ya bajeti hii.

**106. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia miongozo hiyo pamoja na Ahadi na Maagizo mbalimbali ya viongozi Wakuu wa kitaifa wa nchi, katika bajeti ya Mwaka wa fedha 2026/2027, Vipaumbele Vikuu vya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni kama ifuatavyo:-

i. Kuimarisha miundombinu ya Usafiri wa nchi Kavu, Wizara imepanga kujenga barabara zenye jumla ya kilomita 445.25 Unguja na Pemba. Katika kilomita hizo, kilomita 159.5 ni barabara kuu, kilomita 82.73 ni barabara za Mjini, kilomita 156.82 ni barabara za Vijijini/Ndani na kilomita 46.2 ni barabara zinazounganisha maeneo ya Utalii (hoteli) ili kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika kwa urahisi pamoja na kuvutia wawekezaji.

ii. Kuendelea kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali kwa kuziba mashimo, kuzifanyia usafi pamoja na kununua mashine na vifaa vya kusafishia.

iii. Kuimarisha miundombinu ya kuondolea maji ya mvua yaliyotuwama kwa kujenga misingi/Mitaro katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Zanzibar.

iv. Kuimarisha miundombinu ya Usafiri wa Anga kwa kuendelea na Ujenzi wa miundombinu ya Viwanja vya Ndege ikiwemo ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, kuendelea na ujenzi wa jengo la 2 la Abiria (Terminal

2) Awamu ya Pili pamoja na ujenzi wa maegesho ya ndege (Apron) katika Uwanja wa AAKIA.

v. Kuimarisha miundombinu ya Bandari ikiwemo kuendelea na Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani, Bandari ya Abiria na Mizigo katika eneo la Mpiga Duri pamoja na bandari nyengine ili kuimarisha huduma za Usafiri wa Baharini.

vi. Kuimarisha Usalama wa Usafiri barabarani kwa kuweka Kamera za Usalama Barabarani za Kisasa, Uwekaji wa Taa za barabarani, udhibiti wa maeneo ya hifadhi ya Barabara (road reserve), Uwekaji wa Alama za Usalama Barabarani, kujenga njia za watembea kwa miguu na kujenga madaraja ya kuvukia watembea kwa miguu (Pedestrian bridges) katika maeneo ya msongamano wa watu ili kupunguza ajali za barabarani.

vii. Kutayarisha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali itakayowezesha kusimamia na kutoa huduma bora kwa jamii katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi hapa Zanzibar.

viii. Kuanzisha Kampuni ya Ndege ya Zanzibar pamoja kuanza maandalizi ya uwanzishwaji wa usafiri wa umma kwa njia ya reli.

## H.2. PROGRAMU ZA WIZARA NA MALENGO YA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027.

**107. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Programu Kuu tatu (3) ambazo ni:-

- P01- Programu ya Ujenzi na Miundombinu ya Barabara;
- P02 - Programu ya Miundombinu na Huduma za Uchukuzi; na
- P03 - Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi;

108. **Mheshimiwa Spika,** Programu kuu zilizoainishwa katika bajeti hii zimewekewa malengo makhususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbalimbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa kupitia Sekta Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi. Maelezo ya Programu hizo ni kama ifuatavyo:-

**P01- PROGRAMU YA UJENZI NA MIUNDOMBINU YA BARABARA.**

109. **Mheshimiwa Spika,** Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika Programu hii ni kuongezeka kwa mtandao wa barabara pamoja na huduma za ujenzi zilizobora, salama na endelevu zinazopelekea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na jamii nchini. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu Kuu ya Ujenzi na Miundombinu ya Barabara itakuwa na programu ndogo mbili ambazo ni:-
Usimamizi wa Miundombinu ya Barabara, na Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.

**S0104-Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Barabara.**

110. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Wakala wa Barabara Zanzibar. Lengo la Programu hii ni kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya barabara iliyo bora na ya kisasa Unguja na Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia Programu hii, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

111. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu hii ndogo imepanga kusimamia utekelezaji wa miradi ifuatayo: -

i. Kuendelea na ujenzi wa barabara kuu Unguja na Pemba; miongoni mwa Barabara zinazoendelea na zitakazoanza kujengwa ni:- Barabara ya Tunguu – Makunduchi 48 km, Fumba – Kisauni 12 km, Barabara ya Chake – Mkoani km 43.5, Barabara ya Mwera – Dole – Mfenesini 14.3 km, Dunga – Kilombero – Kinyasini 19.0 km, Mkokotoni – Kinazini Junction - Nungwi 18 km, Tunguu – Dunga Jumba la Mawe 7.0 km, Mfenesini – Bumbwini 7 km, Amani – Dunga 12.7 km, Paje – Michamvi 18 km, Chake Chake – Wesha 7.4 km, Barabara Chwale – Kilindini – Konde Sokoni 24.4 km na Kilindini – Micheweni 5.2 km. Kwa ujumla ujenzi wa Barabara Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 umetengewa kutumia jumla ya **TZS 554,500,000,000.**

ii. Kuendelea ujenzi wa Barabara za ndani na Vijijini Unguja na Pemba ikiwemo barabara zinazoingia katika maeneo ya Mahotel ya Kitalii. Miongoni mwa barabara hizo ni Barabara ya Muyuni – Nungwi 13.3 km, ChanjaMjawiri – Tundauwa km 12 na Machomane – Wawi – Vitongoji km 8, Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya **TZS 151,721,177,000.**

iii. Kuendelea na matengenezo ya barabara za Mjini ikiwemo barabara ya Kariakoo – Magomeni – Mwanakwerekwe 2,7 km, Maruhubi – Karakana – Mtopepo 1.4 km, Mtoni – Bububu – Chuwini 6.2 km na Amani – Mikunguni - Biziredi 2.5 km pamoja na kujenga madaraja ya kuvukia watembea kwa miguu (Pedestrian bridges). Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu ya matengenezo ya barabara za Mjini imepangiwa kutumia jumla ya **TZS 95,000,000,000.**

iv. Kuanza maandalizi ya Ujenzi wa Daraja la Charawe – Chwaka kwa kufanya Upembuzi Yakinifu. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,000,000,000.**

v. Kujenga barabara zinazoingia katika Mji wa Michezo Fumba zenye urefu wa kilomita 63.8. Barabara zitakayojengwa chini ya Mpango huu ni Barabara inayoanzia Mazizini (ZRA) - Kisauni – Kombeni – Fumba yenye urefu wa 18.9 km, Fuoni – Kisakasaka – Kombeni yenye urefu wa 8.7 km na Barabara za ndani zinazoingia katika eneo la michezo Fumba zenye urefu wa 4.4 km ambazo zitakuwa na njia sita (Six lanes). Aidha, jumla ya kilomita 31.8 zilizosalia zitajengwa ndani ya mji wa michezo wa Fumba ili kuwa na muunganiko mzuri wa huduma za usafiri. Lengo ni kuhakikisha Zanzibar inakuwa na miundombinu bora ya usafiri inayokidhi vigezo vya kuwa mwenyeji wa mashindano ya mpira wa miguu ya Afrika (AfCON). Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya **TZS 269,079,843,000.**

vi. Kuendelea na ujenzi wa mitaro ya kuondolea maji ya mvua katika mji wa Zanzibar. Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 30,000,000,000.**

vii. Kuimarisha miundombinu mbalimbali itakayosaidia kukuza uchumi katika miji ya Unguja na Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 162,500,000,000.**

**112.** **Mheshimiwa Spika,** Orodha ya Barabara zilizopangwa kujengwa katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 zinaonekana katika **Kiambatanisho Namba 8** na orodha ya maeneo yatakayojengwa mitaro ya kuondolea maji ya mvua katika mji wa Zanzibar yanaonekana katika **Kiambatanisho Namba 9**

**113.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Barabara imepanga kutumia jumla ya **TZS 1,309,001,020,000** kwa ajili ya utekelezaji

wa miradi ya maendeleo Unguja na Pemba, ikiwa **TZS 377,000,000,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **TZS 932,001,020,000** zitatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

**114.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Barabara imepanga kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali Unguja na Pemba kama ifuatavyo:-

a. Kuendelea na kazi ya utunzaji wa barabara ya lami (Routine Maintenance for Paved roads) kwa kufanya ununuzi wa mashine na vifaa vya kusafishia barabara, mitaro na madaraja.

b. Uwekaji wa Mabango 1,000 na viguzo 12,000 vya mipaka ya hifadhi ya barabara Unguja na Pemba.

c. Kurejesha na Uwekaji wa Michoro, Alama na Kingo za Barabarani kwa barabara kongwe na mpya kwa Unguja kilomita 400, Pemba kilomita 150 na Kingo (Guardrail) mita 1000.

d. Kuendelea na matengenezo ya barabara (Routine Maintenance) kwa kuziba mashimo kwa barabara zilizojengwa kwa lami kwa mita za mraba 15,000 kwa Unguja na Pemba.

e. Matengenezo ya dharura Unguja na Pemba.

f. Usimamizi wa uwekaji wa Taa za Kuongozea vyombo vya Moto kwa Unguja na Pemba (Trafic light).

g. Ujenzi wa Ofisi Kuu ya Wakala pamoja na ukarabati wa Ofisi za Kanda.

h. Usimamizi na udhibiti wa hifadhi ya barabara kwa uondoshaji wa vibanda na shughuli zisizo rasmi pembezoni mwa Barabara.

i. Ujenzi wa banda la kuhifadhia malighafi za ujenzi na vifaa pamoja na ulipaji wa fidia kwa eneo la uchimbaji wa kifusi Kibele.

j. Utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Barabara Zanzibar (Zanzibar Roads Master Plan).

k. Kujenga na kukamilisha barabara za Bandamaji Awamu ya Pili kilomita 2.6, Kiboje -Uchukuni kilomita 4.5, Mchangani – Msikitini kilomita 1.3, Kwale – Gongo kilomita 1.0

l. Kufanya matengenezo ya zana na mitambo pamoja na ununuzi wa vipuri.

m. Kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu matumizi ya miundombinu ya barabara kupitia vipindi vya redio na TV.

**115. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wakala wa Barabara Zanzibar imepangiwa kutumia jumla ya **TZS 50,653,960,000** kwa kazi za kawaida na matengengenezo ya barabara Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo, **TZS 4,573,960,000** ni mishahara, **TZS 880,000,000** ni matumizi mengineyo. Aidha, **TZS 45,200,000,000** ni kwa ajili ya utunzaji na ukarabati wa barabara.

**116. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu wa Barabara inaombewa kutumia jumla ya **TZS 1,314,454,980,000** kwa kazi za kawaida, Ruzuku na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia Programu hii.

**S0105 – Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.**

**117. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Wakala wa Majengo. Lengo la Programu hii ni kuhakikisha kuwa Sekta ya Ujenzi inakuwa na ubora, usalama na yenye mazingira endelevu. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027,

Wizara kupitia Taasisi inayosimamia Programu hii ndogo, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

**WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR.**

**118. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo kupitia Programu hii ndogo imepanga kuendelea kutoa huduma za Ushauri Elekezi kwa miradi mbali mbali ya ujenzi wa majengo ya Serikali. Malengo mengine ni pamoja na: -

i. Kuandaa nyaraka za ujenzi na BoQ 39, kati ya nyaraka hizo, 24 zitaandaliwa kwa upande Unguja na 15 zitaandaliwa kwa upande wa Pemba.

ii. Kufanya mapitio ya nyaraka za ujenzi na BoQ 12 kwa nyaraka ambazo hazijaandaliwa na Wakala wa Majengo.

iii. Kusimamia miradi 51 ya ujenzi, kati ya miradi hiyo 36 itasimamiwa Unguja na 15 itasimamiwa Pemba.

iv. Wakala wa Majengo kwa kushirikina na Wizara imepanga kukamilisha mchakato wa uandaaji wa Sheria ya Wakala wa Majengo Zanzibar.

**119. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027, Wakala wa Majengo imepangiwa kutumia jumla ya **TZS 5,736,560,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 1,981,560,000** ni mishahara na **TZS 3,755,000,000** ni matumizi mengineyo.

**120. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo inaombewa kutumia jumla ya **TZS 5,736,560,000** kwa kazi za kawaida kwa taasisi inayosimamia Programu hii.

## P02 - PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA UCHUKUZI.

**121.** **Mheshimiwa Spika,** Matokeo yanayotarajiwa katika Programu hii ni kupatikana kwa miundombinu na huduma za uchukuzi (Nchikavu, Anga na Baharini) zilizo bora, salama na endelevu zinazopelekea ukuaji wa shughuli za uchumi na kijamii nchini. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Kuu ya Miundombinu na Huduma za Uchukuzi itakuwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni; Usimamizi wa Miundombinu ya Uchukuzi (Anga na Baharini) na Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama.

### S0201-Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Uchukuzi (Anga na Baharini).

**122.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Lengo la Programu hii ni kuimarisha miundombinu ya usafiri wa Anga na Baharini ili iwe bora na ya kisasa itakayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa Unguja na Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, katika kutekeleza Programu hii ndogo, kazi zifuatazo zimepangwa kutekelezwa: -

i. Kuendelea na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuongeza urefu wa barabara ya kutua na kurukia ndege, njia ya kupitia ndege pamoja na maegesho ya ndege (runway, taxi way and apron), kujenga jengo jipya la abiria (Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800) na zinazolingana. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 144,500,000,000.**

ii. Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Abiria (Terminal II) Awamu ya Pili pamoja na kujenga jengo Jipya la Kuongozea Ndege (Control Tower) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa AAKIA. Kwa Mwaka wa Fedha

2026/2027, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 30,000,000,000.**

iii. Kuendelea na ujenzi wa Maegesho ya Ndege (Apron) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Kurume. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 36,000,000,000.**

iv. Kuendelea na ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani pamoja na kuweka miundombinu katika eneo la bandari. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 225,500,000,000.**

v. Kuendelea na ujenzi Bandari ya kisasa ya abiria katika eneo la Maruhubi. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 40,000,000,000.**

**123.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Uchukuzi (Anga na Baharini) inaombewa kutumia jumla ya **TZS 476,000,000,000** kwa kazi za maendeleo kwa taasisi inayosimamia Programu hii.

**S0202 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama.**

**124.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari. Programu hii ina lengo la kuimarisha huduma bora na usalama katika Sekta ya Uchukuzi Unguja na Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia Programu hii, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI.**

**125.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya

Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuanza maandalizi ya uanzishwaji huduma za Usafiri wa Reli Zanzibar kwa kufanya Upembuzi Yakinifu. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,000,000,000.**

ii. Kuendelea na kazi ya uwekaji wa taa za barabarani Unguja na Pemba Mijini na Vijijini. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **TZS 8,000,000,000.**

**126.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama imepangiwa kutumia jumla ya **TZS 9,000,000,000** kwa ajili ya kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Programu hii.

## WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

**127.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuziimarisha Karakana za Serikali kupitia Ubiya na Kampuni Binafsi (PPP) ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma kwa kufanya matengenezo ya magari hadi kufikia 2,700 Unguja na Pemba pamoja na kutoa Ushauri wa kitaalamu wa ununuzi na uuzaji wa magari hadi kufikia taasisi 60.

ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kwa kuendelea kuwapatia wafanyakazi wa nne (4) mafunzo ya muda mrefu na 20 ya muda mfupi.

iii. Kukamilisha mchakato wa kuandaa Sheria mpya ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ili iweze kutoa huduma bora zitakazopelekea kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato.

iv. Kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya kiufundi katika Karakana ya matreketa kwa lengo la kubadilisha teknolojia za kiufundi ili kuendana na wakati.

v. Kuandaa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma na taarifa zinazohusiana na Wakala.

**128.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2026/2027, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama imepangiwa kutumia jumla ya **TZS 3,372,360,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TZS 1,360,540,000** ni mshahara na **TZS 2,011,820,000** ni matumizi mengineyo.

**129.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Usafirishaji na Usalama inaombewa kutumia jumla ya **TZS 12,372,360,000** kwa kazi za kawaida, Ruzuku na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia Programu hii.

## P03 - PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

**130.** **Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Programu hii ni kuimarika utendaji wa Wizara pamoja uratibu wa huduma na miradi ya maendeleo katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kwa uwazi na ufanisi. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

**S0301 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji**

**131.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, lengo la Programu hii ni kuimarisha uwezo na ufanisi katika utendaji wa Wizara.

**132.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu hii itaendelea kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuendelea kusimamia masuala ya kiutumishi na uendeshaji wa Wizara ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi na kuwapatia vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuendelea kuvifanyia matengenezo vyombo vya usafiri.

ii. Kutoa makala na machapisho mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli na mafanikio ya Wizara pamoja na kuratibu safari za kikazi za ndani ya nchi na nje ya nchi.

iii. Kuwajengea uwezo watendaji ili kuongezea ujuzi, ufanisi na tija kwa wafanyakazi wa Wizara wa Unguja na Pemba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa kuzingatia mpango wa mafunzo wa Wizara na;

iv. Kuhakikisha kuwa mali za Wizara zinasimamiwa na kutumika kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa.

**133.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji inaombewa kutumia jumla ya **TZS 3,856,600,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 1,956,600,000** ni mishahara na **TZS 1,900,000,000** ni matumizi mengineyo.

### S0302 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

**134. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; lengo la Programu hii ni kuimarisha mifumo ya kisera, mipango, sheria na kanuni za udhibiti katika Wizara.

**135. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya Barabara, Bandari na Viwanja vya Ndege pamoja na kuratibu na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

ii. Kuratibu na kufanya tafiti zinazohusu Sekta za Wizara ikishirikiana na taasisi zilizochini ya Wizara na Sekta Binafsi.

iii. Kutayarisha Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa kazi za Wizara.

iv. Kufanya mapitio ya Sera ya Usafiri Zanzibar, Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar ili iendane sambamba na mabadiliko ya wakati pamoja na kutayarisha Sera ya Ujenzi itakayotoa muongozo wa namna ya kuisimamia sekta hiyo.

v. Kutoa mafunzo ya utayarishaji wa bajeti kwa watendaji wa Wizara kulingana na miongozo kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inayotolewa kila mwaka.

vi. Kukusanya na kuchambua takwimu za maendeleo ya sekta na kuweka mpango bora wa utunzaji wa kumbukumbu za takwimu.

vii. Kusimamia na kuratibu mapitio ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kuzifanyia marekebisho ili ziendane na mahitaji na mabadiliko yaliyopo kwa sasa.

viii. Kuratibu na kuandaa vikao vya mashirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi (SJMT) na Wizara ya Uchukuzi (SJMT).

ix. Kuratibu na kusimamia mashirikiano ya kisekta, Kikanda na Kimataifa ikiwemo kushiriki mikutano mbalimbali inayoandaliwa kuhusu kujadili maendeleo ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi.

x. Kuratibu na kusimamia Taasisi na Mashirika yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara.

**136.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara inaombewa kutumia jumla ya **TZS 1,539,840,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 710,000,000** ni mishahara na **TZS 829,840,000** ni matumizi mengineo.

**S0303 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba**

**137.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba; lengo la Programu hii ndogo ni kuhakikisha uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba zinafanyika kwa ufanisi.

**138.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi Kuu Pemba kupitia Programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa watendaji ikiwemo kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu za uendeshaji wa Ofisi, kufanya matengenezo ya Jengo la Ofisi, ununuzi wa Vifaa vya kufanyia kazi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao.

ii. Kuwajengea uwezo watendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

iii. Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara kwa upande wa Pemba.

**139.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inaombewa kutumia jumla ya **TZS 1,349,960,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **TZS 550,000,000** ni mishahara na **TZS 799,960,000** ni matumizi mengineyo.

## I. HITIMISHO

**140.** **Mheshimiwa Spika,** Kabla sijamaliza hotuba yangu hii sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa wajumbe watatoa michango ambayo itasaidia Wizara kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya kuwahudumia wananchi wetu na hatimae kuipitisha Bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zilizopangwa katika kila Programu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**141.** **Mheshimiwa Spika,** Pia naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kudumisha Amani na Umoja wa nchi yetu. Jambo ambalo linachochea Maendeleo kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema yeye na familia yake ili aendelee kutuongoza kwa mafanikio makubwa.

**142. Mheshimiwa Spika,** Mafanikio katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi ambayo nimeyaeleza kwa kina katika hotuba hii, ni matokeo ya ushirikiano wa wadau wa sekta hizi ndani na nje ya Wizara wakiwemo; Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Wananchi kwa ujumla. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote waliotoa michango mbalimbali ya hali na mali na wale walioshiriki moja kwa moja katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Shukrani za kipekee ninaziwasilisha kwenu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa ushauri na michango mnayoitoa ambayo imewezesha Wizara kuimarisha utendaji katika kutoa huduma za Ujenzi na uchukuzi kwa Wananchi.

